Kesi

Sehemu ya Maandiko, nalo somo langu usiku huu ni kuninii. . .nafikiri Yesu Kristo hakufanyiwa kesi ya haki katika mahakama ya Hero—Hero—Herode, mbele ya Pilato. Siamini alifanyiwa kesi ya haki. Nami nafikiri, katika dakika arobaini na tano zijazo, hebu na tumfanyie kesi, kwa sababu anashukiwa tena. Na sasa ninii . . .

2 Moja ya mambo makuu anayoshukiwa, ni Neno Lake. Sasa ninaamini Neno hilo. Kwa hiyo, ni—nitasoma usiku wa leo kutoka sehemu inayobishaniwa sana katika Maandiko. Hiyo ni Marko, mlango wa 16.

3 Na sasa, kama tulikuwa tukitoa heshima kwa bendera, ama kama tulikuwa tukisikiliza *Bendera Iliyopambwa Kwa Nyota*, tungesimama sote. Nami nafikiri kama tunaweza kufanya hivyo katika kumbukumbu ya nchi yetu nzuri tuliyo nayo, hakika inatupasa kufanya hivyo kwa Neno la Mungu. Kwa hiyo hebu tusimame, kwa muda mfupi tu, wakati ninaposoma kutoka kwenye Neno.

4 Marko, mlango wa 16 wa Marko Mtakatifu, kuanzia kifungu cha 9. Na tusikilize kwa makini wakati tukisoma vifungu hivi. Sasa, tuko moja kwa moja kwenye ule wakati wa ufufuo. Tuko kwenye wakati ambapo Bwana wetu alikuwa ndio kwanza afufuke katika wafu, na alikuwa akionekana, pia, katika sura mbalimbali, kwa watu. Sasa, kifungu cha 9 kinaanza hivi.

> *Naye alipofufuka alfajiri siku ya kwanza ya juma, alimtokea kwanza Mariamu Magdalene, ambaye kwanza alimtoa pepo saba.*
>
> *Huyo akashika njia akawapasha habari wale waliokuwa pamoja naye, nao wakali wanaomboleza na kulia.*
>
> *Walakini hao waliposikia kama yu hai, naye amemwona, hawakusadiki.*
>
> *Baada ya hayo akawatokea watu wawili miongoni mwao, ana sura nyingine; nao walikuwa wakishika njia kwenda shamba.*
>
> *Na hao wakaenda zao wakawapa habari wale wengine; wala hao hawakuwasadiki.*
>
> *Baadaye akaonekana na wale kumi na mmoja walipokuwa wakila, akawakemea kwa kutokuamini kwao na ugumu wa mioyo yao, kwa kuwa hawakuwasadiki wale waliomwona alipofufuka katika wafu.*

Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.

Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.

Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;

Watashika nyoka;. . .hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa,. . .nao watapata afya.

Basi Bwana Yesu, baada ya kusema nao; akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu.

Nao wale wakatoka, wakihubiri kote kote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo. Amina.

5 Sasa na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi, kwa ajili ya maombi. Nami nitawaomba, ikiwa ni sawa, kwamba ikiwa ndugu, Marvin Smith, aliyekuwa mwema sana kwetu jana, naye alinialika kwenye mstari wa maombi pamoja naye jana usiku, kama atamwomba Mungu baraka juu ya Maneno ambayo ndio kwanza niyasome.

6 Ndugu Smith, tafadhali. [Ndugu Marvin Smith anaomba—Mh.] Lijalie, Bwana. Ndiyo, Bwana. Lijalie, Bwana. Lijalie, Bwana. Lijalie, Bwana. Ndiyo, Bwana. Lijalie, Bwana. Amina.

Asante. Mwaweza kuketi.

7 Wengi sana wa rafiki zangu hapa, ambao ningetaka kuwataja wote, ila, kama tu vile ndugu alivyosema, hatuna wakati wa kufanya hivyo. Ndugu Outlaw pale, ndugu rafiki yangu msiri sana kutoka Phoenix, na Ndugu Moseley na—na wengi sana mbalimbali ambao ni vigumu kupata wakati wa kumtambua kila mmoja. Bali nina hakika mnaelewa, sitaki kuwapita.

8 Sasa, kwenye Neno hili, tunakabiliwa usiku wa leo. Nami nataka tu kusema mambo machache kuhusu Andiko hili. Kila twendako, tunapata hili, lililo ninii sana. . .ninii. . .ambapo asiyeamini hukosoa.

9 Hapa wakati fulani uliopita. . .Wengi wenu mnamfahamu Perris Reidhead. Yeye ndiye rais wa Misheni za Sudan. Hiyo ni moja ya misheni kubwa sana za kimsingi duniani. Yeye pamoja na Don. . .Siwezi kukumbuka jina lake la mwisho. Yeye ndiye mchungaji, moja ya makanisa makubwa ya Kibaptisti huko Chattanooga. Alikuja nyumbani mwangu, hu—huko Jeffersonville, na kusema, "Ndugu Branham," kasema, "tunasikia kwamba wewe ulikuwa Mbaptisti."

10 Nami nikasema, “Naam, bwana. Nilifanywa kasisi, Kanisa la Kimishenari la Kibaptisti.”

Akasema, “Ninasikia unashirikiana na Wapentekoste.”

Nikasema, “Naam, bwana. Mimi ni mmoja wao.”

11 Naye akasema, “Vema, ninataka kukuuliza jambo fulani.” Kasema, “Hao wanadai kuwa na Roho Mtakatifu.” Kasema, “Je! unafikiri huyo ni Roho Mtakatifu?”

Nikasema, “Naam, bwana.”

12 Akasema, “Vema, jambo pekee nisiloweza kufahamu, huko kupiga mayowe hayo yote na kupiga makelele na kufanya yasiyofaa namna hiyo.”

13 Nikasema, “Vema, ikiwa wewe—ikiwa wewe huwezi kuufanya mvuke ufingirishe gurudumu, watautoa kwenye filimbi. Hivyo tu.” Nikasema, “Kama—kama wangeweza . . . Hiyo ndiyo sababu niko pamoja nao.” Nikasema, “Laiti ungaliweza tu kukitumikisha kitu hicho, na hiyo, shauku, kwenda huko ng’ambo kuwavuta watu, ingaliuteka ulimwengu.” Lakini nikasema, “Hiyo ndiyo sababu niko huko.”

14 Akasema, “Vema, nilipokuwa mvulana mdogo,” akasema, “Nilipata wito kutoka kwa Mungu. Naye mama yangu akafua nguo kwenye ubao wa kufulia, apate kunipeleka shule.” Kisha akasema, “Mimi, wakati, niliwazia, nilipopata B.A. yangu,” kasema, “hapo nitampata Kristo, lakini,” kasema, “Si—sikumpata.” Ndipo akasema, “Sasa, Ndugu Branham, nina digrii na digrii za heshima za kutosha kuukandika ukuta wako.” Basi akasema, “Kristo yu wapi katika hizo zote?”

15 Nikasema, “Mimi siye, ndugu, nikiwa na elimu ya msingi, kusema hao—hao waalimu walikosea. Bali,” nikasema, “walikuwa sahihi katika yale waliyosema, bali hawakuwa . . . Kuna mengi zaidi ya Hayo.”

16 Naye akasema, “Hii ndiyo sababu ya mimi kuwa hapa.” Akasema, “Shuleni, tulimwelimisha mvulana mzuri wa Kihindi kutoka India. Nafikiri alisoma apate kuwa ninii . . . nafikiri ilikuwa, labda, ilikuwa uhandisi wa ujenzi ama—ama kitu fulani, alikuwa—alipata shahada ya uzamili. Alikuwa akirudi kwenda kuwasaidia watu wake.” Akasema, “Nilimpeleka kwenye—kwenye mashua, ama garimoshi, ambapo ilimpasa kwenda kuabiri mashua, naye apate kurudi India. Nikasema, ‘Mwanangu, wakati ukininii—wakati unaporudi . . .’ Kasema, ‘Sasa umehitimu, na umepata elimu yako, rudi kwa watu wako.’ Kasema, ‘Mbona usimchukue Mungu halisi aliye hai unaporudi, na kumsahau huyo nabii aliyekufa, Muhammad, mnayemwabudu?’”

17 Mvulana huyo, akiwa ni Mwislamu, “Vema,” akasema, “bwana,” akasema, “Yesu wako anaweza kunifanyia nini zaidi ya yale nabii wangu anayoweza kufanya?”

18 "Vema," akasema, "Yesu we—we—we—wetu anakupa Uzima. Nabii wako hawezi."

19 Akasema, "Lakini aliahidi kufanya hivyo." Naam. Akasema, "Unajua, kile sisi Waislamu tunachongojea, ni kuwaona ninyi Wakristo mkifanya yale kiongozi wenu alisema mngefanya."

Akasema, "Ni yapi hayo?"

20 Akasema, "Vema, nanii wenu . . ." Kasema, "Unaona, Muhammad aliahidi tu uzima baada ya mauti. Lakini," kasema, "Yesu aliahidi ya kwamba mambo aliyofanya Yeye ninyi nanyi mtayafanya."

Ndipo akasema, "Loo," kasema, "vema," akasema, "unaona, walizifanya."

Akasema, "Ati hao? Tunanena kukuhusu wewe, wewe sasa."

21 Akasema, "Vema, sasa, bwana," akasema, "Nakwambia." Kasema, "Je! umesoma Agano Jipya?"

Kasema, "Loo, mara nyingi, tena na tena."

Akasema, "Kwa mfano, hivi unarejea kwenye Maandiko yapi?"

22 "Vema," akasema, "mahali pengi, Yohana 14:12, na kadhalika," akasema, "Marko 16."

23 Akasema, "Vema, sasa," akasema, "unaona, Marko 16," kasema, "tunasoma kwamba, kwa kweli, baadhi ya Maandiko haya, kwamba hayajathibitishwa." Akasema, "Marko 16, kuanzia kifungu cha 9 na kuendelea," anasema, "haipatikani kwenye—kwenye miswada ya kale zaidi." Akasema, "Iliongezewa tu."

24 Sasa, kweli, sijui mnalipata hilo wapi, ikitokea kwamba kuna mkosoaji karibu. Mbona, nimesoma historia ya Biblia kwa miaka ishirini. Mnaona? Hakika. Ireneo na Polycarp, na hao wote, walilitambua. Mnaona? Hakika. Hakika iliongezewa. Vatikani haikuiamrisha. La hasha. Bali huyu, hawa waandishi halisi, walisema Yesu alisema Haya, Maandishi yaliyothibitishwa.

Na kwa hiyo akasema, "Kuanzia kifungu cha 9 na kuendelea, Haijavuviwa."

25 Huyo Mwislamu akasema, "Vema, basi, Bw. Reidhead, ni sehemu ipi iliyovuviwa basi?" Akasema, "Nataka ufahamu kwamba Kurani nzima imevuviwa, sio tu sehemu *hapa* na sehemu *pale*." Ni kushindwa kwa jinsi gani! Kwa hiyo akasema, "Vema," akasema, "vema, kama—kama sivyo, ikiwa sehemu hiyo haijavuviwa, ninajuaje kama hiyo nyingine yote haijavuviwa?" Sasa, hiyo hapo ninii nzuri . . .

26 Akasema, "Vema," kasema, "wakati, Yesu alifufuka katika wafu; naye Muhammad yumo kaburini."

27 Akasema, “Ati Yeye amefufuka kutoka kaburini?” Akasema, “Yeye alisema, kama alifufuka, ‘Angekuwa ndani yenu, hata mwisho, na kazi alizofanya mngezifanya pia.’”

28 Ndipo Bw. Reidhead akaniambia, kasema, “Ndugu Branham, sikujua la kusema.”

Akasema, “Mbona, Yesu kweli alifufuka katika wafu!”

29 Kasema, “Mmekuwa na miaka elfu mbili kulithibitisha, na asilimia tisini ya ulimwengu karibu haijui lolote kulihusu.” Kasema, “Hebu Muhammad afufuke, nao ulimwengu mzima utajua hilo katika saa ishirini na nne.” Hiyo ni kweli. Endapo mmekuwa kaburini mwake, baadhi yenu wamishenari, kila saa nne wanabadilisha zamu ya farasi pale, farasi mweupe, ambaye atampanda, ulimwenguni, atakapofufuka katika wafu.

30 “Bali haitubidi kungojea Yesu afufuke katika wafu. Yeye tayari amefufuka katika wafu.”

31 Kwa hiyo akasema, “Lithibitishe. Yeye aliahidi hilo, kama alifufuka katika wafu.” Kwa hiyo akasema, “Vema, unajuaje?”

Akasema, Bw. Reidhead akasema, “Anaishi moyoni mwangu.”

32 Naye akasema, “Pia Muhammad yuaishi moyoni mwangu.” Kasema, “Bw. Reidhead,” kasema, “Dini ya Kiislamu inaweza kutoa saikolojia chungu nzima sawasawa na Ukristo.”

33 Akasema, “Ndipo nikaona aibu, Ndugu Branham, kama Mkristo aliyeshindwa. Basi nikajiahidi ya kwamba ningekuja, nikazungumze nawe.” Mnaona?

34 Mbona, Biblia hiyo yote imevuviwa. Mungu hulilinda Neno Lake. Mungu hana budi kuuhukumu ulimwengu siku moja.

35 Na endapo atauhukumu kwa kanisa, atauhukumu kwa kanisa lipi? Akiuhukumu kwa kanisa Katoliki (ninyi Wakatoliki mngesema hivyo), ni kanisa Katoliki lipi, basi, la Othodoksi ya Kiyunani, la Kirumi, ama lipi? Akiuhukumu kwa la Kibaptisti, ninyi Methodisti mmepotea. Akiuhukumu kwa la Kimethodisti, ninyi Baptisti mmepotea. Akiuhukumu kwa la Kipentekoste, nyote wawili mmepotea. Mnaona? Yeye hatauhukumu kwa kanisa lolote.

36 Atauhukumu kwa Yesu Kristo, Naye Yesu Kristo ni Neno. Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza, ilisema, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu.” Kwa hiyo, Yeye atauhukumu kwa Yesu Kristo, na Yeye ni Neno. Biblia ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

37 Mungu akiwa asiye na kikomo, hapo mwanzo, kwa hekima yake isiyo na kikomo, maarifa Yake, aliigawanya Injili Yake katika kila wakati. Tunaona ya kwamba makanisa yanalivuruga kabisa, ndipo Mungu anamtuma nabii Wake jukwaani. “Nalo

Neno la Bwana humjia nabii." Wanajuaje ndilo? Ndilo dhihirisho la U—Ujumbe wa wakati huo. Sasa, wakati, kile . . .

38 Musa alipokuja, kama ilivyoahidiwa ya kwamba angekuja, vipi kama angalikuja na ujumbe wa Nuhu? Usingefaa kitu. Musa asingaliweza kujenga safina kwa ajili ya kuwaokoa watu. Neno la Mungu lililoahidiwa kwa ajili ya wakati wa Musa lilikuwa ndilo Neno lililopaswa kuthibitishwa.

39 Katika wakati wa kila mwonaji na kila nabii, imekuwa ni vile vile, bali tunawaona watu wakiishi katika mn'gao wa nuru nyingine. Kama Yesu alivyosema, "Mnazipaka rangi kuta ama makaburi ya manabii, nanyi ndio mliowaweka mle." Mnaona? Mnaona, wanajenga kitu fulani, juu ya ujumbe, na kuishi kwenye huo mng'ao wa nuru hiyo, na kukataa kutembea katika nuru iliyo ya wakati huo.

40 Hiyo ndiyo sababu walikataa kumjua Yesu Kristo hapo alipokuja. Hiyo ndiyo sababu Yesu aliwasihi, akisema, "Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, Nayo Ndiyo yanayonishuhudia." Bali walikuwa na kanuni nyingi sana za imani na kadhalika, na mapokeo yao, hata Yesu akasema, "Mmelitangua Neno la Mungu, kwa mapokeo yenu." Na hivyo ndivyo imekuwa katika kila wakati.

Mungu atauhukumu ulimwengu kwa Yesu Kristo.

41 Na mara nyingi, mnaona, jambo ni kwamba, sisi watu hujaribu kuwa na fasiri yetu wenyewe ya Neno, kusema, "Marko 16, kuanzia kifungu cha 9 na kuendelea, haijavuviwa."

42 Ni kwa nini haijavuviwa? Mungu hahitaji mfasiri yeyote. Yeye Ndiye anayejifasiria. Mungu hujifasiria Mwenyewe. Nayo Biblia ilisema, "Si ya kufasiriwa apendavyo mtu yeyote."

43 Mungu alisema, hapo mwanzo, "Iwe nuru," ikawa nuru. Hilo halihitaji kufasiriwa.

44 Alisema, "Bikira atachukua mimba," naye akachukua. Hilo halihitaji fasiri yoyote. Alichukua. Ingawa, alipoichukua, kwenye wakati alipoipata, watu walikuwa wamejaa sana kanuni za imani hata hawakulielewa. Lilipita moja kwa moja juu ya vichwa vyao.

45 Limefanya hivyo katika kila wakati, nalo litafanya hivyo tena. Sasa, tunaona, hiyo ni kweli. Watu hufanya hivyo. Kristo na kanisa . . . Tunaona, katika siku hii tunayoishi, hakuna kitu tofauti na siku nyingine yoyote. Watu, kanisa, sikuzote wanamsifu Mungu kwa yale aliyofanya, na sikuzote wakisema yale atakayofanya, na kudhihaki yale anayofanya. Hiyo daima imekuwa ndiyo historia ya kanisa, na ndivyo ilivyo usiku wa leo. Ni kwa sababu nadharia za kujibunia huingia Humo na kuitatanisha kabisa. Ndipo Neno la kweli linapojitetea, mnaona,

hao wamejaa sana kanuni za imani, mpaka wamepofushwa sana na mng'ao huo, hawawezi kulikubali.

46 Mbona, sababu ambayo Walutheri, ambayo Wamethodisti, wakati ninyi Wamethodisti...Mvulana huyu mzuri wa Kimethodisti, hapa, ndio kwanza aimbe muda mfupi uliopita. Wakati mvulana huyo, ninii . . . Sababu ilikuwa ni nini? Mnaona, Walutheri walikuwa wakiishi katika mng'ao wa Luther, na hiyo ndiyo sababu ujumbe wa Kimethodisti haukukolea vema. Na Wapentekoste walipokuja, wote walikuwa wakiishi katika mng'ao wa Methodisti, mpaka Pentekoste ikaja. Lakini, mnaona, yote haya, kama mtayachunguza tu Maandiko, mwangalie nyakati za kanisa na yale kila mmoja utakayofanya, mtaona mahali hasa tunapoishi. Tunaishi kwenye wakati huu.

47 Sasa, juu ya msingi wa ukosoaji huu, mwingi sana, wa Neno la Mungu, ninataka kuchukua fungu hili usiku huu, na kuliita: *Kesi*.

48 Yesu hakufanyiwa kesi ya haki katika siku za Herode, katika siku za Pilato. Lakini, katika siku hii, ninataka kuona, usiku wa leo, kwenye kundi hili dogo la watu, endapo mtaketi pamoja nami, ninataka kuhakikisha kwamba Yeye anafanyiwa kesi ya haki. Kwa sababu, Yeye angali ni Neno. Angali ni Neno. Ni wangapi wanaokubaliana na hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Nalo Neno lingali ni Mungu. "Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Kwa hiyo, hebu tuhakikishe kwamba anafanyiwa kesi ya haki.

49 Sasa, nitaifanya hii kama mahakama, mkinivumilia. Ninajua linasikika kama lisilo la kawaida, bali sisi ni kusanyiko dogo tu hapa sasa, ambapo tunataka kulileta Neno hili, ambalo ninadai ni Neno la Mungu. Nami nipo hapa kulitetea. Na sasa, tutalileta kwenye kesi ya mahakamani, kama tu ilivyokuwa hasa katika siku ambapo Herode alimfanyia kesi, ama Pilato, mbele ya mahakama ya Pilato. Tutamleta mbele ya mahakama kwenye chumba hiki cha Ramada, huu mwaka wa 1964, Aprili ishirini na saba, 1964.

50 Sasa tutakifanya hiki kuwa mahakama. Nanyi ndio hakimu na baraza la wazee wa mahakama; ninyi, mahakama. Mimi nitakuwa msimamizi wa mahakama. Nasi tutaifanya hii kama kesi ya mahakamani. Na mwishowe, mjiamulie, kama ninii lolote—kama baraza lolote la wazee linavyopaswa kutoa uamuzi kwa ajili ya hukumu. Ndipo basi tendo lenu, tangu sasa na kuendelea, litaonyesha ulio uamuzi wenu. Haidhuru mnasema nini sasa, tendo lenu litathibitisha uamuzi wenu. Sasa, shtaka ni kwamba, leo, enyi marafiki . . .

51 Mimi nitafanya kazi ya msimamizi, sasa, na jinsi ingekuwa katika shtaka halisi la mahakamani, na kumfanyia mashtaka, kama mtanivumilia kwa muda mfupi na kuniombea.

52 Sasa, shtaka ni, Neno la Mungu dhidi ya ulimwengu, ulimwengu ambao hauliamini. Nalo shtaka ni: Neno la Mungu dhidi ya ulimwengu. Ki—kinachosababisha shtaka, ni, uvunjaji wa ahadi. Hiyo ni kusema, uvunjaji wa ahadi ndio uliosababisha shtaka hili.

53 Na sasa, nasikia kwamba katika kesi ya kawaida ya mahakamani, kwamba mwendesha mashtaka sikuzote huiwakilisha serikali. Nafikiri hiyo ni kweli. Katika mahali hapa, mwendesha mashtaka anauwakilisha ulimwengu. Naye wakili mwendesha mashtaka ni Shetani, naye anauwakilisha ulimwengu katika mahakama hii hapa alasiri ya leo.

54 Naye Mshtakiwa ni Mungu, Neno Lake, kwa kuwa Mungu daima ni Neno. Mnaona?

Naye Shahidi wa utetezi ni Roho Mtakatifu.

55 Naye shahidi wa wakili mwendesha mashtaka ni Bw. Asiyeamini, Bw. Mwenye Kushuku, na Bw. Mkosa Subira. Hawa watatu wanakuja kama shahidi wa wakili mwendesha mashtaka, ambaye ni Shetani, anayeuwakilisha ulimwengu.

56 Sasa hebu tuikumbushe mahakama hii nidhamu. Na sasa hebu tumwite mwendesha mashtaka, hebu na amwite shahidi wake wa kwanza kizimbani, kutoa ushahidi dhidi ya Neno.

57 Na sasa sikilizeni kwa makini. Sasa, huenda nisiweze, katika kuharakisha, nikijaribu kumaliza huu katika dakika thelathini ama arobaini, huenda nikaruka kitu fulani. Lakini nikiruka, Roho Mtakatifu na akifunue sasa, wakati mahakama inapokumbushwa nidhamu.

Kumbukeni, ninyi ni hakimu na baraza la wazee wa mahakama pia.

58 Na sasa mwendesha mashtaka anamwita shahidi wake, shahidi wa kwanza, kizimbani, atoe ushahidi. Naye anamwita Bw. Asiyeamini, naye anasimama kizimbani, kutoa ushahidi. Basi Bw. Asiyeamini anadai ya kwamba Neno lote la Mungu, la ahadi za Mungu, si la kweli. Hilo ndilo lalamishi lake, kwamba Neno la Mungu haliwezi kutumainiwa, lote. "Sehemu Yake ni sawa. Bali lote . . . " Yeye anadai kwamba ni mwaminio, Bw. Asiyeamini. Bali anadai kwamba ni mwaminio, naye anasema, kwamba, "Neno lote la Mungu haliwezi kutumainiwa. Si la kweli."

59 Anadai ya kwamba alitembelea mkutano unaosemekana ni wa Roho Mtakatifu, ambapo watu walikuwa wakidai Marko 16 ni Kweli. Na watu wengi walidai kwamba walikuwa wameponywa, wakati, ambapo inasema katika Marko 16, "Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Naye mtu huyu asema ya kwamba alidai kuwa alimwamini Mungu. Alimsikiliza huyu anayejiita mhubiri wa Roho Mtakatifu,

naye...kundi hili la Roho Mtakatifu lililokuwa likitoa kila namna ya shuhuda.

60 Naye alikuwa mgonjwa mwilini mwake, ndipo akawekewa mikono na watu hawa kwenye mkutano huu wa Roho Mtakatifu. Na hiyo ilikuwa ni miezi miwili iliyopita, wala hakuna hata kitu kimoja kimetukia bado. Yeye ni mgonjwa tu kama alivyokuwa wakati alipowekewa mikono. Hajabadilika, hata kidogo. Ni mgonjwa tu kama alivyokuwa. Kwa hiyo, anasema, kwamba, "Mungu hana haki, kuweka Andiko kama hilo katika Biblia, huku akiwa hana uwezo wa kulitekeleza. Si halali kwa Marko 16 kuwa katika Biblia," kwa maana ati anathibitisha kwamba Mungu halitimizi Neno Lake. Naye anataka kumshtaki Mungu kwa ajili ya kuweka ahadi kama hiyo katika Neno Lake. Vema. Tutamwomba aketi chini.

61 Na sasa tutamwita Bw. Mwenye Kushuku afuate aje huku, akatoe ushahidi. Bw. Mwenye Kushuku anasimama kizimbani. Naye anasema kwamba atasema kweli. Anadai kwamba ni mwaminio. Naye alisema alikuwa mgonjwa muda mrefu, kwamba ana madhara ya kutokana na ugonjwa mbaya aliokuwa nao. Ndipo akamsikia mtu fulani akishuhudia mtaani, kwamba ana mchungaji mtauwa. Naye mchungaji huyu wa kanisa hili alihubiri na kusema ya kwamba, Yakobo 5:14, "Mtu wa kwenu, akiwa hawezi, na wawaite wazee wa kanisa. Nao na wawapake mafuta na kuwaombea. Kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Mungu atawainua. Kama walitenda dhambi yoyote, watasamehewa. Ungameni dhambi zenu, mmoja kwa mwingine. Na mwombeane, kwamba kuomba kwa mwenye haki kwafaa sana, mkiomba kwa bidii."

62 Basi alisema kwamba alipanda kule, kama mwaminio. Anataka kuiambia mahakama hii hivi, kwamba, "Nilipanda nikaenda kule kwa uaminifu wote, na nilikuwa na huyu anayejiita mchungaji mtauwa wa kanisa hili, ambaye wengi walidai hilo, alipowapaka mafuta na kuwaombea. Naye mchungaji alisema, yeye mwenyewe, ya kwamba Mungu alilijibu Neno hilo, na hilo Neno la Yakobo 5:14 lilikuwa ni la kweli. Na kulikuwa na wengi wakishuhudia kwamba lilikuwa ni kweli." Lakini alipanda kule, naye mchungaji, mtauwa, akampaka mafuta, kulingana na Yakobo 5:14, akamwombea. Na hiyo imekuwa ni miezi sita iliyopita, wala hajapata matokeo yoyote, hata kidogo. Yeye ni mgonjwa tu kama alivyokuwa hapo mwanzo.

63 Kwa hiyo, Bw. Mwenye Kushuku anasema ya kwamba Hilo haliwezi likawa ni kweli. "Marko 16 si kweli, wala Yohana, ni—ni Yakobo 5:14. Si la kweli, kwa kuwa Mungu hushindwa kulitimiza Neno Lake. Kama hili ni Neno la Mungu, basi Mungu anashindwa kutimiza Neno Lake, maana, kwa uaminifu, kama mwaminio, alienda na kumwacha mchungaji, ambaye hao wengine walidai waliponywa naye, ampake mafuta na

kumfanyia vile vile alivyowafanyia hao wengine. Na, miezi sita iliyopita, wala hajapata matokeo yoyote ya wakati wowote. Kwa hiyo, yeye pia anataka kumshtaki Mungu, kwa kuweka ahadi za kijinga kama hizo katika Neno Lake, ambazo hatazizingatia."

64 Kesi inapamba moto hapa, sivyo? Acha aketi chini, Bw. Mwenye Kushuku.

65 Sasa, shahidi anayefuata ni Bw. Mkosa Subira. Yeye ni mhuni. Sasa yeye atapanda juu, naye atatoa ushuhuda wake. Basi anatangaza msimamo wake, kwamba, siku moja wakati akisoma Injili ya Marko, mlango wa 11. . . Sio wa 16, sasa. Mlango wa 11, kifungu cha 22 na 23, ambayo inasema hivi, "Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka', wala usione shaka moyoni mwako, ila uamini kwamba hayo usemayo yatatukia, yatakuwa yako. Na uombapo, amini kwamba utapokea uliyoomba, yatakuwa yako."

66 Alisema amekuwa kilema miguuni mwake, alitembea kwa magongo kwa yapata miaka ishirini na mitano. Basi wakati akisoma Andiko hili, naye alikuwa amefunzwa na mchungaji wa—wake, kwamba Maandiko yote yalitolewa na Mungu na yalikuwa yamevuviwa. Kwa hiyo, kama aliuambia mlima huu, "Ng'oka," wala asione shaka, bali aamini ya kwamba aliyosema yatatimia, yangekuwa yake. Na alipoomba, aamini kwamba amepokea alichoomba, atapewa.

67 Sasa, anasema aliomba, na kwa uaminifu wote. Naye akasema angeweza kuweka magongo yake chini na kutembea kutoka mahali hapo. Naye, kwa uaminifu, kwa moyo wake wote, aliamini ya kwamba kile alichokuwa amesema kilikuwa ni kweli. Naye . . . Hiyo ingekuwa ni karibu miaka mitano iliyopita, naye ni kiwete tu kama alivyowahi kuwa. "Sasa, kama Mungu basi," yeye anasema, "angetimiza Neno Lake, basi kwa nini asilitimize Neno Lake?"

68 Sasa, ninatoa tu vifungu vitatu vya Maandiko pale, ama mashahidi watatu, bali nitamwacha mwendesha mashtaka awaite wengine zaidi. Sasa tutaacha . . .

69 Bw. Asiyeamini, yeye alishuhudia. Bw. Mwenye Kushuku, yeye alishuhudia. Asiyeamini alishuhudia; Marko 16. Naye Bw. Mwenye Kushuku alishuhudia dhidi ya Yohana, ama Yakobo 5:14.

70 Naye Bw. Kukosa Subira, yeye alishuhudia dhidi ya Marko 11, Yesu Mwenyewe akinena. Na Marko 11:22 na 23, yeye alishuhudia dhidi ya hilo. Sasa tutamwomba Bw. Kukosa Subira aketi chini.

71 Sasa, kama vile sisi sote, kwa njia moja ama nyingine, tumekuwa mahakamani. Sasa, mwendesha mashtaka hana budi kuikazia kesi yake. Kwa hiyo Mwendesha Mashtaka anapanda juu, kuikazia kesi yake. Yule anayeuwakilisha (samahani) ulimwengu, Shetani, anasimama kizimbani. Kwa hiyo anadai,

kwenye mahakama hii, alasiri ya leo, ama jioni ya leo. Anataka . . . Mwendesha mashtaka, ibilisi, anaitaka mahakama hii kufahamu ya kwamba watu hawa ni waaminio, na kwamba Neno hili kweli limeandikwa katika Neno, "Neno la Mungu, linavyodaiwa," anasema, kwamba jambo hili limeandikwa. Naye anadai ya kwamba linatoka mahali mbalimbali katika Maandiko. Nao watu hawa ni mashahidi kwamba sivyo ilivyo.

72 Naye anataka kuiambia mahakama hii, mwendesha mashtaka anataka, kwamba anataka mahakama hii ifahamu ya kwamba Mungu hana haki, kuweka ahadi za kijinga kama hizo, katika Kitabu, watoto Wake waaminio wapate kuzikubali; halafu hana uwezo wa kuzishughulikia, kudhihirisha kile alichoahidi angefanya. Naye ana mashahidi watatu hapa. Nao mashahidi watatu ni thibitisho, kama tujuavyo, katika Maandiko yote. Naye ana mashahidi watatu, kutoka mahali patatu mbalimbali katika Maandiko, kwamba Mungu hana haki ya kuweka vitu kama hivyo katika Neno Lake, kusudi watoto Wake wapendwa waliangalie, na kujaribu kulikubali na kuliamini kama Yeye alivyosema, kisha Mungu anawavunja moyo, bila kujali.

73 Pia, a—anadai kwamba watoto hawa, kwa uaminifu wote, wanafanya jambo hili, watu hawa, nao wameshindwa. "Watoto wa kweli waaminio wameshindwa na Neno la Mungu, linavyodhaniwa kuwa. Kwamba wanayadai mambo haya kwa kuwa yameandikwa katika Kitabu hicho, na mtu mwingine aliyaingiza mle ndani, wala si Neno la Mungu. Wala Biblia haiwezi kuaminika. Kwa kuwa, haya hapa mahali patatu na shuhuda tatu kuthibitisha ya kwamba ni uongo." Sasa anajenga hoja yake. Kwa kuwa, yeye, mwendesha mashtaka, anataka kuelekeza, kuuvutia usikivu wa mahakama hii, kwamba watu hawa hapa walilikubali Neno hili kwa uaminifu, wakiamini lilikuwa ni Neno la Mungu, Naye Mungu ameshindwa kuiheshimu imani yao.

74 Isitoshe, anataka kudai kwamba hao ni waaminio, kwa kuwa wanasema wao ni waaminio. Hata hivyo, tena, mwendesha mashtaka anataka kugeukia, kuuvutia usikivu wa mahakama hii alasiri ya leo. Hata hivyo Mungu anaahidi tena, katika mahali pengine kwenye Maandiko, ya kwamba mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio. Na imeandikwa. Hilo ni shtaka jingine. Mambo yote, haidhuru ni nini, mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio. Nao watu hawa wanadai kwamba ni waaminio. Ninaitaka mahakama ifahamu, mwendesha mashtaka aliye kizimbani sasa anaikaza kesi.

75 "Hata hivyo, tena, Yeye anadai kuwa hai baada ya kufa Kwake, kwamba Yesu anadai kuwa hai baada ya kufa Kwake. Basi mwendesha mashtaka anataka kuiuliza mahakama hii, je! mmemwona baada ya kufufuka katika wafu? Yako wapi makovu ya misumari mikononi Mwake? Ipo wapi ile taji ya miiba

iliyowekwa juu Yake? Ziko wapi alama kwenye paji la uso Wake? Na Yuko wapi, ikiwa amefufuka katika wafu?"

76 Ndipo basi, "Tena, Yeye anasema katika Waebrania 13:8, kwamba, Neno Lake linasema ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mwendesha mashtaka anaitaka mahakama hii kukumbuka hilo. Halafu kwenye...Yuko wapi, iwapo Yeye yupo?" Anataka kumwona. Tena, anadai kwamba sivyo ilivyo. Anadai ya kwamba Luka 17:23 sivyo ilivyo. Anadai ya kwamba Ufunuo 3 sivyo ilivyo. Anadai ya kwamba Marko 4 sivyo ilivyo. Anadai ya kwamba Maandiko haya yote ya kufufuka Kwake, kwamba ni uongo mtupu. Anataka kuonyesha hilo, kwamba ni uongo.

77 "Na pia anadai ya kwamba mbingu na nchi zote zitapita, bali si hata nukta moja wala yodi kutoka kwenye Neno Lake itashindwa." Naye mwendesha mashtaka anawataka mfahamu, enyi mahakama, alasiri ya leo kwamba ana mashahidi hapa wa kuthibitisha kwamba wamekosea. Sasa, anaiomba mahakama kuzingatia hili, wakati tukiwazia.

78 Sasa, tunamuuliza mwendesha mashtaka sasa iwapo amemaliza kujenga hoja yake, kuyanukuu Maandiko; akidai kwamba si ya kweli, akishuhudia kwamba Hayo si ya kweli, kwamba hayajavuviwa. "Hayana faida. Hayawezi kutegemewa. Hayawezi kuaminika." Ana mashahidi wa kuthibitisha kwamba Hayo hayawezi kuaminika. Sasa tuna kesi kweli kweli mkononi mwetu.

Sasa, hebu tumwache mwendesha mashtaka na mashahidi wake waketi chini.

79 Sasa tutamwita Shahidi wa utetezi, ambapo Shahidi wa utetezi ana haki ya kutetea...ama kumtetea mshtakiwa. Na sasa Shahidi wa utetezi, ambaye ni Roho Mtakatifu, hebu na apande hapa juu, tupate kusikia ushuhuda Wake.

80 Jambo la kwanza, sasa, kwa kuwa mmesikia yale mwendesha mashtaka aliyosema. Mmesikia yale yeye, mashahidi wake waliyosema. Mmeyasikia Maandiko. Mmeyasikia yakisomwa. Nao hawa hapa mashahidi, kwamba Hayo si ya kweli.

81 Sasa, Roho Mtakatifu, kama nisemavyo, ambaye Ndiye Shahidi wa utetezi, anaitwa. Jambo la kwanza, Yeye anataka kuita...Shahidi wa utetezi, Roho Mtakatifu, anataka kurejea kwenye kesi ya mahakama hii, kwamba mwendesha mashtaka halifasiri Neno, vizuri, kwenu. Anataka kuuvutia usikivu wenu, pia, kwamba mwendesha mashtaka huyu anayewapa fasiri ya Neno, ambaye anauwakilisha ulimwengu na kutokuamini, ni mfasiri yule yule ambaye Hawa alikuwa naye hapo mwanzo. A-ha. Yeye alilifasiri Neno vibaya, kidogo tu.

82 Sasa, huenda nikasimama hapa, mahakamani, kwa muda mfupi tu, kusema hili. Kama Mungu alisababisha maradhi haya yote na huzuni na mauti juu ya nchi, kama ilimbidi kufanya

hivyo kwa sababu ya haki Yake, kulitimiza Neno Lake, Yeye hawezi kuwa mwenye haki na asitimize Neno Lake. Hana budi kulitimiza Neno Lake, apate kuwa mwenye haki. Inaupasa utakatifu Wake. Inampasa Yeye. Na kama Hawa, sio tu . . .

83 Shetani hakunii, mwendesha mashtaka, hakufasiri vibaya kitu hicho chote. Yeye alifasiri vibaya Neno moja tu, ama kitu kama hicho, nayo ikasababisha mauti kuipiga dunia nzima. Na kila hospitali, kila king'ora kilichowahi kulia, kila—kila kifo kilichopata kufiwa, kila pambano, kila mtu kwenye uwanja wa vita, kila maskini, mtoto mchanga, mgonjwa, anayeteseka, na wote hao, ilisababishwa na kutokuamini Neno moja tu la Neno la Mungu. Na kama ilisababisha yote haya, kwa sababu ya kutokuamini Neno moja, utarudije, ukikosa kuamini Neno moja?

84 Inabidi pawe na kitu fulani ambacho Mungu hana budi kuuhukumu ulimwengu kwacho, na hicho ni Yesu Kristo, Neno. Hatuna budi kuliamini lote.

85 Angalieni. Yeye alisema kwamba yeye, kwamba, "Watu hawa wamekuwa wakisikiliza fasiri mbaya ya Neno. Mwendesha mashtaka si ninii . . . analifasiri vibaya, ana—analifasiri Hilo vibaya, kwenu, kama tu vile alivyofanya kwa Hawa. Ahadi ni kwa ajili ya waaminio peke yao; sio wanaojifanya waaminio, wenye kushuku, ama wakosa subira. Ni kwa waaminio tu. Na iwapo . . .

86 Hebu niseme jambo hili. Kama kuna mtu anayepaswa kujua kama jamaa hawa ni waaminio ama sio, anapaswa kuwa ni Shahidi wa utetezi, kwa kuwa Ndiye anayelihuisha Neno. Mnaona? Yeye . . . Ni kama tu mwili wako, mwili wako ni kipande cha nyama. Lakini isipokuwa roho iwe mle ndani, kuuhuisha mwili huo, umekufa. Na vivyo hivyo Neno, limekufa, isipokuwa Roho Mtakatifu alihuishe Neno hilo. Na kama Yeye Ndiye mwenye kulihuisha Neno, anapaswa kujua kama jamaa hawa kweli ni waaminio ama sio. Nafikiri tunaye Shahidi mzuri wa utetezi. Anapaswa kujua kama ni kweli ama si kweli. Kwa maana . . . Yeye ni Shahidi mzuri wa utetezi kwa kuwa Yeye Ndiye anayelihuisha Neno.

87 Tena, Shahidi wa utetezi anataka kuuvutia usikivu wa—wa Neno ambalo linashukiwa hapa, ambalo ndio kwanza tusome, kwamba mwendesha mashtaka anajaribu kupata hoja ya mashtaka dhidi ya Neno. Shahidi wa utetezi anataka kuuvutia usikivu wenu, kwamba halikuweka wakati wowote wa ukombozi. Kamwe hakusema ni lini. Alisema tu, "Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Hakusema kwamba wataruka papo hapo. Neno halisemi hivyo. Yakobo 5:14 ilisema, "Wakati utakapopakwa mafuta," alisema, "kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa huyo, naye Mungu atamwinua." Halikusema wataruka juu papo hapo. Halikusema.

Marko 16 haikusema wataweka mikono juu ya wagonjwa na patatokea mwujiza. Alisema tu, "Watapata afya." Liliahidi.

88 Sasa, angalieni kama kumekuwako na baadhi ya hawa wasioamini wamekuwa wakiwafasiria Neno vibaya, wakisema, "Vema, *huyu* aliombewa. Kwa nini hakuamka? Nilikuwako kwenye mkutano huo. Kamwe sikuona kitu kikitendeka." Mnaona mfasiri huyo waliye naye? Mnaona kile wanachosikiliza?

89 Shahidi wa utetezi anataka kuionyesha mahakama hii, alasiri ya leo, kwamba Neno halikusema wangeruka juu papo hapo. Alisema, "Watapata afya." Hilo ndilo aliloahidi. Kamwe hakuweka wakati wowote. Na hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya waaminio pekee.

90 Pia Shahidi wa utetezi anataka kuuvutia usikivu wenu hapa, alasiri ya leo katika mahakama hii, kwamba Neno la Mungu limetajwa, na Yesu Kristo, kuwa ni Mbegu. Nayo mbegu inaweza tu kukua inapoanguka penye udongo mzuri kuihuisha mbegu. Na kama Mbegu hii ikianguka kwenye udongo, na umerutubishwa na imani, hauna budi kuihuisha. Bali ikiwa hamna kitu mle . . .

91 Ni kama vile ungalitaka kupewa damu. Ukaenda kwa tanipu, ukatundika tyubu ndani yako na katika tanipu, utapataje damu? Hamna damu mle.

92 Si zaidi sana Neno la Mungu linavyoweza kamwe kuhuishwa katika moyo wa asiyeamini ama wa mwenye kushuku. Haina budi kuanguka ndani ya imani halisi inayoamini kwamba mbingu na nchi zitapita, bali Neno hilo halitashindwa kamwe, kama vile Ibrahimu, ambaye aliviita vitu visivyokuwapo, kana kwamba vipo; alitumaini pasipokuwa na matumaini. Alimwamini Mungu.

93 Sasa tunaona ya kwamba huyu Shahidi wa utetezi anataka kuwatazamisha jambo hili, ya kwamba Neno ni Mbegu ambayo mpanzi alipanda. Imeandikwa katika Maandiko, ya kwamba Neno ni Mbegu. Nayo mbegu haina budi kuanguka. Nayo Maandiko yanasema, "Zingine kweli zilianguka penye udongo wenye miamba, nao ndege wa angani wakaziokota. Zingine zilianguka muda mrefu kutosha tu kuotesha mizizi ya kutosha kuchipuka, nayo miiba na michongoma ikazisonga. Bali zingine kweli zilianguka penye udongo mzuri, na ikazaa mia." Anataka kuwatazamisha jambo hilo.

94 Naye anataka kusema, kwamba, "Kama Neno hili, kwenye mkutano huu wa Roho Mtakatifu, ambapo watu walikuwa wakiwekewa mikono, linatumika tu kwa waaminio. Hakuna ahadi humu ndani ila utengano wa Milele kutoka kwa Mungu, kwa wasioamini. Ni kwa waaminio tu!"

95 Mtu fulani aliniambia, sio muda mrefu uliopita, kasema, "Sijali ni vipi. Siamini mimi."

96 Nikasema, "Bila shaka huamini. Si la wasioamini. Ni la waaminio, hao wanaoamini."

97 Sasa, mashahidi wa utetezi, Shahidi wa mshtakiwa, hasa, anataka kumwita shahidi. Ana haki ya kuwaita mashahidi, pia. Kwa hiyo Shahidi wa utetezi anataka kumwita shahidi Wake wa kwanza dhidi ya jambo hili, na kwa ajili ya Neno.

98 Tutamwita Nuhu jukwaani, alasiri ya leo, mbele ya mahakama hii, atoe ushuhuda kwa ajili ya Mshtakiwa. Nuhu alikuwa mkulima wa kawaida tu, bali alikuwa ni nabii. "Nalo Neno la Bwana huwajia manabii." Biblia ilisema hivyo. Naye Nuhu aliishi, anataka kushuhudia kwamba aliishi katika wakati wa kisayansi sana, ulio mkuu kuliko ule tunaoishi sisi sasa. Aliishi katika wakati ambapo waliweza kujenga piramidi, wangejenga sfiniksi, ambazo hatuwezi sisi. Hatuna mitambo ya kuzijengea. Basi Nuhu aliishi katika wakati mkuu, na aliishi katika wakati wa sayansi.

99 Ndipo anasema kwamba Neno la Mungu lilimjia, akiisha kuwa nabii aliyethibitishwa, kwamba Neno la Bwana lilimjia na kusema, "Andaa safina, kwa kuwa itanyesha." Huku haikuwa imenyesha, katika historia yote ya ulimwengu. Na juu ya ushuhuda wake na kumtetea Mungu, basi alisema Mungu alimwambia hivyo, "Na wote waliokuwa nje ya safina hii wataangamia."

100 Nao wanasayansi wangeweza kurusha vyombo mwezini, katika siku hiyo, kwa rada yao na kadhalika, kwa kuwa Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu," wakati wa namna ile ile. Yeye alisema wangeweza kuthibitisha kwamba hakukuwako na mvua kule juu, na kwamba Bw. Asiyeamini hapa, na Bw. Mwenye Kudhihaki, na Bw. Mwenye Kushuku, kwamba daima walimfuatilia na kumdhihaki, kwa kuamini jambo la kijinga kama hilo. Walikuwa, walidai kwamba ni waaminio huko nyuma, bali yeye alisema, "Mungu hakusema kitu kama hicho."

101 Hata hivyo, yeye alikuwa ni nabii, nalo Neno la Bwana likamjia na kumwambia afanye hivyo. Ndipo akaanza, kuitayarisha safina. Akajiandaa, na kuijenga safina. Akiisha kuikamilisha safina; na Bw. Mwenye Kushuku, na Bw. Mkosa Subira, na hao wengine wakiizunguka-zunguka safina.

Unaona, unasema, "Hivi hao waliishi huko nyuma?"

102 Sikilizeni, Mungu humchukua mtu Wake, bali kamwe si Roho Yake. Roho aliyekuwa juu ya Eliya, alikuja juu ya Elisha, na kuendelea, na kuendelea. Roho aliyekuwa juu ya Yesu, alikuja juu ya Kanisa, na kuendelea, na kuendelea.

103 Naye ibilisi humchukua mtu wake, bali kamwe si roho. Roho yuyo huyo, roho wa kidini, anaendelea kuishi, kama yule aliyekuwa juu ya Mafarisayo. Yupo papa hapa Tucson, Arizona, akiwa asiyeamini tu, na ninii tu—na mshika kanuni za imani

tu na—na mwenye mapokeo kama huyo alivyokuwa. Sio hapa Tucson tu, yuko kote ulimwenguni.

104 Na vivyo hivyo Roho Mtakatifu ni halisi tu usiku wa leo kama alivyokuwa wakati wowote, Yesu Kristo.

105 Angalieni. Anataka kusema ya kwamba watu hawa walimdhihaki, kwa kuwa m—m—m—m—mshamba hivyo, asiye na akili zaidi wala maarifa zaidi ila kuamini kwamba maji yangeshuka kutoka mahali pasipokuwapo na maji, wala hayajawahi kuanguka. Lakini, hata hivyo, Nuhu alisema alisimama imara na kuamini kwamba ingenyesha, kwa kuwa Mungu alisema hivyo. Alijua ya kwamba Mungu aliweza kufanya lolote ambalo alisema angefanya, kwa hiyo akaijenga safina.

106 Basi baada ya kuikamilisha safina, aliketi mlangoni pa safina. "Nao wakasema, 'Sasa, ewe mlokole,' Bw. Asiyeamini, Bw. Mwenye Kudhihaki. Shahidi wa utetezi . . . Ama, mashahidi wa mwendesha mashtaka." Akasema, "Walipitia karibu nami. Nao wakasema, 'Sasa safina yako imejengwa. Sasa umeiwekea milango. Basi iko wapi mvua yako?' Lakini ilionekana mbaya sana," akasema, "wakati mwingine. Lakini, hata hivyo, nilijua ya kwamba Mungu aliweza kulitimiza Neno Lake. Hakusema itanyesha lini. Alisema itanyesha. Na ilikuwa ni hayo tu. Hakusema ni lini itakaponyesha. Yeye alisema tu itanyesha. Nami nilijua itanyesha, kwa maana aliniagiza kuijenga safina. Nami nikasimama imara."

107 Ndipo tunaona kwamba, tarehe kumi Mei, aliingia ndani ya safina, asubuhi moja, nao mlango ukafungwa nyuma yake, na hakuna mtu angaliweza kuufungua.

108 Basi Bw. Asiyeamini, Bw. Mwenye Kushuku, walitembea kuizunguka safina na kumcheka na kumdhihaki, na kusema, "Sasa, ewe mzee mpumbavu, uliufunga mlango huo, nami nafikiri unakusudia tuamini ya kwamba kitu Fulani kiliufunga. Tunazijua hila zako. Wewe si kitu ila mchawi. Nawe ni mmoja tu wa jamaa kama hawa hapa wanaojaribu kufanya vitimbi. Na ni namna fulani ya udanganyifu. Nawe uliufunga mlango."

109 "Lakini," akasema, "katikati ya hayo yote, nilikuwa pale. Niliuona mkono wa Mungu ukiufunga mlango."

110 Halafu, siku ya kwanza, tutasema, "Tutaona ikinyesha." Siku ya kwanza, haikunyesha. Siku ya pili, haikunyesha. Siku ya tatu, haikunyesha. Na kuendelea, hata siku ya saba.

111 Nami ningetaka kukomea hapa, kwenye ushahidi wa Nuhu, na kuwajulisha jambo hili, kwamba utakuja wakati ambapo wanaume na wanawake, kanisa, watakuwa wakiendelea moja kwa moja kuhubiri na kuamini wanaokoka, wakati mlango utakuwa umefungwa kama tu vile ilivyokuwa wakati huo. Endapo huko ndani, ingia sasa, maana Mungu ataufunga mlango wala hapatakuwapo na rehema tena. Yeye alisema, "Kama

ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.”

112 Kumbukeni, wakati mmoja hata wanafunzi walimwambia Yesu, “Kwa nini waandishi wanasema kwamba imempasa Eliya kuja kwanza?” hao wanafunzi.

113 Yesu akasema, “Amekwisha kuja wala hamkujua.” Nao wakafahamu ilikuwa ni Yohana Mbatizaji; alikwisha kuwako hapa duniani, na amekwisha kukatwa kichwa na kupaa Utukufuni. Nalo jambo walilokuwa wakilitazamia lilikuwa limepita tayari.

114 Moja ya siku hizi, wanaume na wanawake watalia. Itakuwa mbali mno, imechelewa sana. Mlango utafungwa. Yesu anasema itakuwa hivyo. “Wanawali walikuja na kubisha mlango, na kusema, ‘Turuhusu tuingie.’ Walitaka kupata Mafuta kidogo.” Bali iliwapasa kupata Mafuta hapo Mafuta yalipokuwa yakitolewa. Waliubisha mlango. Lilisema, “Walitupwa kwenye giza la nje ambako kutakuwa na kulia, kuomboleza, na kusaga meno.” Ninajaribu tu kufanya upande huo mdogo wa utetezi, kwa mahakama sasa, wa—wa Neno.

115 Sasa, Nuhu alisema, “Lakini baada ya miaka mia moja na ishirini, asubuhi moja mawingu yalianza kutanda, kisha mvua ikaja. Mungu aliahidi. Hakusema itatukia lini. Walidhani itatukia juma lilo hilo aliponiambia. Nami nilikuwa na imani ingeweza kutukia juma hilo. Nami nilikuwa na hakika nilipoimaliza safina kwamba lingetendeka, bali halikutendeka. Bali nilisimama imara kwa kuwa Mungu alifanya ahadi hiyo. Yeye hakusema tu siku ambayo itanyesha. Alisema itanyesha.” Kwa hiyo, yeye, shahidi anaketi chini.

116 Shahidi wa pili anapanda juu, ambaye ni baba Ibrahimu. Tutamwita. Yeye alisema, “Loo, naam, ninamjua Bw. Mwenye Kudhihaki hapa. Na—namjua Bw. Asiyeamini, Bw. Mwenye Kushuku, loo, yule Bw. Kukosa Subira. Nilikuwa nabii, pia, katika siku zangu. Ndipo Neno la Bwana likanijia na kusema, ‘Jitenge na watu hawa, kwa kuwa utampata mtoto kwa Sara mkeo.’ Alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano, nami nilikuwa na sabini na mitano. Alikuwa amekoma hedhi kwa muda wa karibu miaka ishirini na mitano, thelathini. Nilimwoa. Alikuwa dada yangu wa kambo. Nilimwoa alipokuwa msichana tu, nami mvulana. Tofauti ya miaka kumi katika umri wetu, nami nikamwoa. Akawa mke wangu. Tulikuwa tumeishi pamoja miaka hii yote, naye alikuwa tasa nami mgumba. Na hata hivyo, nikiwa ni nabii, Neno la Bwana lilinijia na kusema, ‘Utamzaa mwana kwa Sara.’”

117 “Vema, nilipomwambia Sara hivyo, alishuka akaenda mjini akanunua kitani na kushona vijibuti, akaweka tayari pini na kila kitu. Ndipo siku ishirini na nane zikapita. Nikasema, ‘Wajisikiaje, mpenzi?’”

118 "Kasema, 'Hamna tofauti.' Lakini nilisimama imara, kwa kuwa nilijua lilikuwa ni Neno la Bwana." Hiyo ni kweli.

119 "Tukaenda kumwona daktari, naye akatufukuza ofisini." Mzee, umri wa miaka sabini na mitano; na mwanamke, miaka sitini na mitano, ati wanaenda kuzaa mto-. . .

120 Mwajua, unapoliamini Neno la Mungu, haidhuru hali yako ikoje, Yeye alifanya ahadi.

121 Naye alisema, "Nilienda kwa daktari, naye daktari akatufukuza ofisini."

122 "'Mzee kama wewe?' Kasema, 'Mwangalieni. Yuna kasoro kidogo kichwani mwake.' Kasema, 'Jamaa huyu mzee ana kasoro fulani.'"

123 Ndipo wenye kudhihaki wakaanza kutembea kila mahali, kasema, "Ibrahimu, yuko wapi yule mwana ambaye ulikuwa umzae kwa Sara, baada ya mwezi wa kwanza? Hana dosari, ndivyo wanavyoniambia." Mwaka wa kwanza ukapita. Hakuna kilichotendeka. "Ibrahimu, baba wa mataifa, una watoto wangapi sasa?" Miaka kumi ikapita, kungali hakuna tofauti. Wenye kudhihaki!

124 "Bw. Mkosa Subira, aliendelea kunielekezea kidole, 'Mnaona, hamna kitu. Mbona, kama kuna kitu kwake, ungekuwa nacho. Hiyo ni miaka kumi iliyopita. Unapaswa uwe umempata mtoto huyo mchanga, katika miaka kumi.'"

125 Lakini, alisema, "Nilisimama imara, kwa kuwa nilishawishika kabisa, hayo ndiyo aliyosema Mungu. Mungu kamwe hakuniambia wakati nitakapompata mtoto huyo mchanga. Alisema nitampata.

126 "Lakini baada ya miaka ishirini na mitano, nilipokuwa na umri wa miaka mia moja na Sara alikuwa na tisini, mtoto huyo akatokea." Yeye ni shahidi mzuri sana. "Nilingojea miaka ishirini na mitano. Sikusita katika ahadi ya Mungu, kwa kutokuamini."

127 Nasi tunadai kwamba tu wana wa Ibrahimu, na hatuwezi kungojea kuanzia usiku mmoja hadi mwingine. Inathibitisha tu kwamba sisi sio. Hiyo ni kweli. Angalieni, tunaingia upande mbaya.

128 "Unaona," alisema, "Nilingojea miaka ishirini na mitano. Mungu hakuniambia, 'Mwezi ujao Sara atapata mimba.' Alisema, 'Utampata mtoto.' Nami nilishawishika kabisa, haidhuru nilizeeka jinsi gani. Nami nilijua ya kwamba nitaliona likitukia, kwa kuwa alikuwa awe ni mtoto wangu. Amina. Hakuna kitakachonidhuru. Uzee, maradhi, mauti, ama chochote kile hakiwezi kunidhuru, mpaka ahadi hiyo itimie. Wala sikusita katika ahadi hiyo, kwa kutokuamini."

129 "Lakini kila siku, wakati Sara aliposema, 'Sijisikii vema zaidi,' nilipata nguvu zaidi. Kila mwaka wakati aliposema,

'Vema, sikumpata mwaka huu.' 'Basi utampata mwaka huu.' 'Sikumpata mwaka uliopita.' 'Tutampata mwaka huu.' Hilo liliendelea zaidi na zaidi, na zaidi na zaidi, mwaka nenda mwaka rudi, kwa muda wa miaka ishirini na mitano. Ndipo siku moja, nikamwona akigeuka kuwa kijana mwanamke. Nikaanza kuona nguvu zangu zikija. Ndipo mtoto akazaliwa, miaka ishirini na mitano baadaye."

130 Neno kamwe halikusema ni wakati gani angemzaa mtoto, bali lilisema atampata.

131 "Ibrahimu, ninajua ungeweza kushuhudia mengi, bali shuka chini. Ninataka shahidi mwingine." Vema.

132 Shahidi wa utetezi sasa atamwita shahidi Wake wa tatu. Huyo atakuwa ni Musa. Naye Musa alisema, "Nilipozaliwa, nilizaliwa nabii." Anataka mjue kwamba karama na miito havina majuto.

133 Haijalishi utasoma vitabu vingapi kutoka kwenye maduka haya, ambavyo vinasema kwamba Mungu hafanyi hivyo, Biblia ingali ni ya kweli, kwamba, "Karama na miito havina majuto." Unazaliwa katika ulimwengu huu, kile ulicho.

134 Na sasa angalieni. Musa, yeye alikuwa na ishara, kushuka kwenda kuwaonyesha watu, na kulikuwako na sauti ya kuifuata ishara hiyo. Hata hivyo, wakati aliposhuka kule na ishara iliyotolewa na Mungu. Sasa, msikose kupata hili, enyi mahakama. Wakati aliposhuka pamoja na ishara hii iliyotolewa na Mungu iliyotoka kwa Mungu, Mchungaji Farao alijaribu ku—kuipaka matope karama yake aliyopewa na Mungu, kwa kumfanya aseme ni uchawi. Alikuwa na mtu fulani ambaye angeweza kufanya jambo lile lile, mchawi fulani. Ndipo akajaribu kuifanya karama aliyopewa na Mungu mbinu duni ya kichawi.

135 Mafarao wote wachungaji hawakufa siku hiyo, mnaona. "Namna fulani ya kuwasiliana kimawazo, namna fulani ya nguvu za Shetani." Na jambo ni kwamba, waliwaita wachawi wa kawaida na kufanya jambo lile lile alilofanya.

136 "Lakini," akasema, "hilo halikunitikisa, kwa kuwa ninajua ya kwamba Sauti iliyosema nami ilikuwa ni Sauti ya Kimaandiko, kwenye mti huo. Akasema, 'Nimesikia vilio vya watu Wangu, Nami nimeona mateso yao, na nimeikumbuka ahadi Yangu.' Nayo Sauti . . . "

137 Ingawa, ilikuwa si kawaida sana katika siku hiyo, kwa jambo kama hilo kutukia. Walikuwa na kila namna ya vitimbi vya kichawi wangaliweza kufanya. Ndipo Mungu akampa kitu fulani, ishara, iliyoonekana kama ni namna fulani ya mbinu duni ya kichawi, kumjaribu mtumishi Wake. Ee Mungu! Lakini, alisimama imara, kwa sababu Sauti iliyomwagiza ilikuwa ni Sauti ya Kimaandiko, naye alijua ilikuwa ni Mungu.

138 Nanyi mwajua, tumeahidiwa kitu hicho hicho katika siku za mwisho, kitu hicho hicho kurudia tena, hao akina Yambre na Yane kurudi, kushindana na Kitu kile cha kweli wakati kikifanya kazi. Bali upumbavu wao utafanywa dhahiri wakati huo. Kwa . . .

139 Kwa hiyo akajaribu kuchukua mwigaji fulani wa kimwili, mtu fulani aliyejaribu, aliyesogea hapo karibu na kujaribu kuiigiza karama ambayo Mungu alimpa, kuifanya ionekane kana kwamba ilikuwa namna fulani ya shughuli duni.

140 Lakini Musa anawataka ninyi nyote mjue, alasiri ya leo, wakati akishuhudia, ya kwamba haidhuru huyo mchungaji alijaribu kuifanya karama yake ionekane kana kwamba ilikuwa ni ya kijanja na namna fulani ya mbinu duni ya kichawi, yeye alijua ilikuwa ni Maandiko, kwa kuwa Sauti ya Mungu ndiyo iliyomwambia. Naye akasimama imara. Basi anawataka . . . kuwajulisha, kwamba ilikuwa ni muda mrefu baadaye, bali Mungu alilitimiza Neno Lake, na kumrudisha moja kwa moja mahali ambapo alisema atakuja, pamoja na wana wa Israeli.

Musa, shuka chini.

141 Hebu Shahidi wa utetezi amwite shahidi mwingine. Basi tutamwita Yoshua. Yoshua ana ushuhuda wa ajabu hapa, ambao angetaka kutoa.

142 Yeye aliwatuliza watu, akasema. Musa alipowaita, mmoja kutoka kwenye kila dhehebu, awatume kwenye—kwenye nchi ya ahadi, ku—kutafuta kujua kama hiyo nchi kweli ilikuwapo ama haikuwako. Walikuwa ndio kwanza waambiwe hilo. Kwa imani walikuwa wametembea umbali huo.

143 Kwa hiyo Musa akamvuta Mpresbiteri, Mlutheri, Mpentekoste, na wote. Akamtoa mmoja wao nje, kila mmoja, na kuwapeleka kwenye nchi ya ahadi. Ndipo wakati wawili wa hao waliporudi na ushahidi, mnajua kilichotukia? Kundi lote likaanza kulitilia shaka. Walipoona upinzani ukiwa ni mkubwa sana, upande huo mwingine ulikuwa ni mkubwa sana, "Mbona," walisema, "tunaonekana kama panzi, tukiwa karibu nao, hao Waamaleki na—na Wahiti, na kadhalika." Kisha wakasema, kwamba, "Sisi—sisi, mbona, tunaonekana kama panzi. Hatuwezi kushinda."

144 Naye Yoshua anataka kushuhudia, "Niliwatuliza watu." Akasema, "Tulieni," huko Kadeshi-barnea, kile kiti cha hukumu. Alisema, "Tulieni, ninyi nyote. Hebu nilete ninii yenu . . . Neno hili, kwenu. Mungu alitwambia, huko chini, kupitia Musa na kupitia . . . ama kupitia Ibrahimu, ya kwamba nchi hii ilikuwa ni yetu. Alituma Nguzo ya Moto miongoni mwetu, iliyosema na nabii wetu hapa katika kichaka kilichowaka moto. Na yale nabii huyu amesema yamekuwa ni kweli. Naye Mungu alitwambia tayari alikuwa ametupa nchi

hii. Tunaweza hata na zaidi kuiteka, maana ni yetu tayari.” Akasema, “Niliwatuliza watu, na kuwanyamazisha.”

145 Lakini mnajua nini? Ilikuwa ni miaka arobaini baadaye kabla hawajaiteka nchi hiyo. Walikuwa na safari ya yapata siku mbili tu, kutoka Kadeshi, wangalikuwa wameingia kwenye nchi ya ahadi.

146 Naweza kusimama hapa kwa dakika moja? Ninyi Wapresbiteri, Wamethodisti, na Wabaptisti, ama ninyi Wapentekoste, miaka hamsini iliyopita tungaliipata Nchi ya ahadi, bali mlianza kuzozana ninyi kwa ninyi, mkifanya madhehebu kutoka upande mmoja, na *huyu* akilipata *hili*, na *huyu* na kulipata *hili*, na ufunuo mpya, badala ya kulifuata Neno. Na sasa tumekuwa ng’ambo hii ya Ahadi kamilifu kwa muda wa miaka hamsini.

147 Lakini, kumbukeni, ilikuwa ni miaka arobaini, bali Yoshua anawataka nyote mjue ya kwamba Mungu alilitimiza Neno Lake, kwa kizazi kipya kabisa. Aliiteka ile nchi ya ahadi jinsi tu ilivyoahidiwa, maana aliwatuliza watu kwenye Neno la Mungu, kuwafahamisha kwamba Mungu alifanya ahadi, kwamba nabii huyu waliyekuwa wakimfuata hakuwa nabii wa uongo, kwa kuwa mambo aliyokuwa akifanya yaliambatana kabisa na Maandiko. Haijalishi Farao alisema ni ya uongo vipi, jinsi wachawi walivyojaribu kusema ni ya uongo, jinsi ambavyo hao wangeweza kufanya jambo lile lile, na kila mtu kufanya jambo lile lile.

148 Basi Yoshua anawataka mjue ya kwamba kulikuwako na mtu fulani mle ndani, aliyetaka kuwafanya dhehebu. Jina lake lilikuwa ni Dathani, naye pamoja na Kora. Nao wakasimama, kasema, “Kuna watu wengi walio watakatifu kukuliko wewe.”

149 Mungu kamwe hayashughulikii makundi. Ni mtu binafsi. Hawezi kubadilika. Kile Mungu afanyacho, mara ya kwanza, hana budi kubaki vivyo hivyo.

150 Hapa, angalieni. Uamuzi wa kwanza wa Mungu kumwokoa mwanadamu ulikuwa ni kwa Damu iliyomwagika ya Mtu asiye na hatia. Haujabadilika kamwe. Mungu kamwe habadiliki. Tumejaribu kuwajengea miji. Tumejaribu kujenga minara. Tumejaribu kuwaelimisha. Tumejaribu kuwaundia madhehebu. Nasi tunaenda mbali zaidi, wakati wote. Kuna mahali pamoja tu ambapo mwanadamu anaweza kushiriki, hapo ni chini ya Damu iliyomwagika ya Mtu asiye na hatia. Hivyo ndivyo tu tukavyopata kuliamini. Jinsi tu tunavyoweza kukukusanyika, ni chini ya Damu iliyomwagika ya asiye na hatia. Mungu kamwe habadilishi njia Yake. Mungu, hata wakati mmoja, kamwe hakushughulika ila na mtu mmoja. Hatakuokoa ati kwa sababu wewe ni Mmethodisti, ama kwa sababu wewe ni Mpentekoste. Atakuokoa kama mtu binafsi, sio kama kundi. Kamwe Yeye

hafanyi hivyo. Yeye huwaokoa watu binafsi, mmoja, mtu mmoja tu ndiye anayejishughulisha naye.

151 Musa alilia mbele za Bwana, Naye Bwana akasema, "Jitenge, Musa. Nilikuita, kwa ujumbe huu." Ndipo akauacha ulimwengu uwameze. Kwa hiyo Yoshua anawataka mfahamu hilo, pia.

152 Sasa, baada ya Yoshua kushuka, tutamwita shahidi mwingine upesi sana, kusudi tusichukue muda mrefu sana. Ninataka kumwita Isaya. Ningeweza kuwaita mamia, bali nitaita tu hawa wachache kisha niondoke.

153 Isaya, nabii, alisema, "Katika siku zangu, Bwana alinithibitisha kama nabii Wake. Nasi tunajua kwamba Neno humjia nabii. Ndipo basi, kila kitu nilichosema, Mungu alikiheshimu na kukifanya kitimie. Tangu nilipokuwa mvulana mdogo, na kuendelea, kila kitu kilichosemwa kilitimia. Nilithibitishwa miongoni mwa watu kama nabii.

154 "Na ndipo siku moja Mungu akanipa kitu kisichoaminika kabisa kusema, ninachoweza kuwazia. Akasema, 'Bikira atachukua mimba. Nitampa ishara kuu. Nitawapa Israeli na ulimwengu ishara kuu. Wanataka ishara, kwa hiyo nitawapa ishara kuu. Bikira atachukua mimba.' Nami, nikiwa nabii aliyethibitishwa, nikifanya kitu kama hicho kisichoaminika, bali ninajua ilikuwa ni sauti ya Mungu."

155 Nanyi mwajua, huenda mkasema jambo hili. Huenda Isaya akaishuhudia mahakama alasiri ya leo, na kusema hivi, kwamba, karibu kila bikira aliyekuwako katika Israeli aliweka tayari nguo za mtoto mchanga, kwa maana atakuwa ndiye msichana aliyekuwa nao. Hiyo ni kweli. Atakuwa ndiye huyo bikira. Kila mmoja wao akajifanya tayari. Na mmoja wao alijua, mwezi ujao atapata mimba . . . kwa bikira. Atakuwa bikira, atachukua mimba, kwa maana Isaya, nabii, alikuwa ni nabii aliyethibitishwa. Chochote alichosema katika Jina la Bwana kilitimia. Na sasa anasema, "Bikira atachukua mimba."

156 Nao wanawake wakawashika wasichana wao wadogo, "Binti yangu ndiye atakayekuwa huyo." Huyo mwingine, *huyu*, *huyu*, mzuri, "Atakuwa wa kundi *hili*. Atakuwa wa kundi *hili*. Atakuwa wa kundi *lile*." Wote hawa, hao, kila mmoja wa binti zao atapata mtoto huyu, kwa kuwa nabii alisema hivyo.

157 Ndipo kizazi hicho kikapita. Isaya akafa. Ahadi haikutimia, ila miaka mia nane baadaye. Mungu hakusema ni lini bikira atakapochukua mimba. Alisema tu atachukua mimba. Anawataka mjue hilo, kwamba Mungu hakusema, "Katika kizazi *hiki*, ama kwenye wakati *huu*, ama wakati *fulani*, ama jambo *fulani*, bikira huyu atachukua mimba." Alisema tu, "Bikira atachukua mimba." Ilikuwa ni miaka mia nane baadaye, lakini huyo bikira alipata mimba. Mnaona? Mungu hudumisha Neno Lake. Mnaamini hilo? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . wakati wowote apate kulifanya.

158 Sasa, ningeweza kuita kila namna ya mashahidi wa utetezi hapa, pamoja na Shahidi wa utetezi, hasa, kutoa ushahidi. Ningeweza kuita watu kutoka hapa nje. Lakini kama—kama mahakama hii itaniwia radhi, naweza kupata majaliwa ya kuwa shahidi anayefuata?

159 Sitazungumza juu ya Musa, na kitu fulani kilichotukia huko nyuma, ama kitu kilichotukia miaka hamsini iliyopita, ama kitu kilichotukia, miaka mia moja iliyopita ama miaka mia tano iliyopita. Nitazungumza juu ya kitu kilichotukia sasa. Ninataka. . .Ninaamini. . .Nami nataka kuwa shahidi anayefuata, kushuhudia leo, kwamba, Neno la Mungu lililoahidiwa kwa ajili ya siku hii; si siku ya Musa, si siku za wanafunzi, si siku ya Luther, si siku ya Pentekoste, sio siku ya Methodisti.

160 Lakini, siku hii, ninataka kuishuhudia, kizimbani. Na kama mtasamehe jambo hili la kibinafsi. Kwa sababu, haina budi kuwa ni ushahidi wa kibinafsi, na hauna budi kuwa ni wa kweli. Kwa sababu, ninajua kwamba ni Nani Yule tunayemtetea, Naye atajua kama ni Kweli ama si kweli.

161 Ninaamini ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho, na ujumbe wa siku nyingine hautafaa siku hii. Hauwezi. Hauna budi kuwa ni Ujumbe wa leo hii, sio wa miaka kumi iliyopita. Ujumbe wa majira haya, Ujumbe wa kizazi hiki, Neno linaunena. Ndipo kama Neno linaahidi, hapana budi kuweko na jambo la kulithibitisha.

162 Na hiyo ndiyo sababu walishindwa kumpokea Yesu alipokuja mara ya kwanza duniani, ni kwa sababu walikuwa wanaishi chini ya mapokeo. Naye Yesu akawaambia, akasema, "Yachunguzeni Maandiko. Yananishuhudia Mimi."

Kasema, "Sisi ni wanafunzi wa Musa."

163 Akasema, "Kama mngalikuwa wanafunzi wa Musa, mngaliniamini Mimi, kwa kuwa Musa aliandika habari Zangu. Tafuteni katika Maandiko."

164 Na hao vipofu, watu wa mapokeo, hata hivyo ni watu wazuri, watu watakatifu, hakuna mtu angaliweza kuwanyoshea kidole. Walikuwa ni makuhani. Waliishi mfano. Walikuwa ni watu usioweza kuwanyoshea kidole, maana, kama ungaliwanyoshea, wangalipigwa mawe. Walikuwa ni watu wazuri. Iliwabidi kuwa watu wazuri, kwa torati. Nao walilelewa, kutoka kizazi kimoja hadi kingine, wana wao na wajukuu, na vitukuu vyao, iliwabidi wote kuwa makuhani, Walawi. Na hata hivyo watu hao, katika mafunzo hayo, ambao hawakujua kitu kingine ila seminari na Biblia, nao walikuwa ni vipofu sana walishindwa kumwona.

165 Inawezekana kwamba tuingie humo tena? Kumbukeni, Maandiko yale yale yalisema tutaingia, hiyo ni kweli kabisa, yalisema tutaingia. Sasa, kama ushuhuda wa kibinafsi. . . Wakati mwingine tunapanga mambo sana, hata tunakuwa

wagumu sana juu ya *hili*, kwamba *hii* ndiyo kanuni ya imani, *hili* ndilo jambo litupasalo kufanya, mpaka tunalikosa maili milioni moja. Nami nafikiri tutafanya jambo lilo lilo, maana Maandiko yalisema tutafanya.

166 Sasa, kama kitu cha kibinafsi, bali msiache liakisi. Natumaini ni kwa sababu tu niko kwenye kizimba cha kushuhudia katika mahakama hii.

167 Ninaamini ya kwamba tuko kwenye ile saa ya Kuja kwa Bwana. Ninaamini ya kwamba matetemeko haya ya nchi na kadhalika tuliyo nayo, huu mwezi ambao wananinii . . . Hapa juu kwenye chumba cha kuangalilia na kadhalika, wanauangalia mwezi huu. Unarusha mlipuko unaoonekana kama damu kutoka ndani yake. Yesu alisema ya kwamba mwezi utageuka kuwa damu, na kutakuwako na matetemeko ya nchi kote duniani, kwenye—kwenye siku hizo kabla ya Kuja Kwake. Alidai kwamba siku hiyo itakuwa hasa kama ilivyo sasa.

168 Nami ninaamini, enyi mahakama, ninataka kuwaambia jambo fulani alasiri ya leo, kwamba, sioni jambo moja la kumzuia asije sasa hivi. Kwamba, ulimwengu, kama ningalikuwa na wakati ningewathibitishia, umekaa kikamilifu, hata kwa majina na mahali pake, jinsi unavyopaswa kuwa umekaa wakati Yeye atakapokuja. Majira hayo ni lini? Sijui. Hakuna ajuaye. Bali Yeye alisema, "Mambo haya yatakapotimia, angalieni juu." Israeli iko kwenye nchi ya uenyeji wake. Kila kitu kimekaa sawa kabisa, kwa ajili ya Kuja Kwake.

169 Sasa, nilipokuwa mtoto mchanga. Watu wangu, hakika, wakiwa ni wa ukoo wa Kiairishi, labda hapo awali tulikuwa Katoliki, bali baba na mama yangu hawakuhudhuria kanisa hata kidogo. Katika nyumba ndogo ya milimani, huko juu kwenye jimbo la Kentucky; asubuhi moja, tarehe sita Aprili, 1909, katika nyumba ndogo ya kale ambayo hata haikuwa na madirisha yoyote; ni kitu fulani kama mlango mdogo, uliingia, uliingiza nuru. Wakati Bwana Yesu aliponiruhusu kuja duniani, nikiwa mzaliwa wa kwanza wa mama na baba yangu; mama akiwa na umri wa miaka kumi na mitano, babangu kumi na minane. Na kwenye foronya ndogo ya manyasi.

170 Nafikiri ninyi watu hapa kamwe hamfahamu foronya ya manyasi ilikuwa nini. Lakini, sisi, ni wangapi walipata kujua foronya ya manyasi ilikuwa nini? Vema, mmetoka sehemu gani ya Kentucky? Mnaona?

171 Kwa hiyo basi, foronya ya manyasi, kwenye foronya ndogo ya manyasi, pamoja na mto wa nyasi kavu, kitanda hicho kimoja kidogo chumbani. Chumba kimoja kidogo, na jiko dogo, ilikuwa tu kama, kitu hicho chote pamoja, kisingekuwa futi ishirini, chote pamoja. Maskini kibanda kidogo cha kale cha magogo, hakijasakafiwa hata kidogo, meza iliyotengenezwa kwa kisiki.

172 Na hapo, katika chumba hicho kidogo, wakati Yesu Kristo aliponiruhusu kuja duniani. Ninaweza tu kusema jambo hili kwa ushuhuda wa wazazi wangu, ambao hawakuwa wa kidini. Bali hawakuwa na taa kama tulizo nazo hapa, si hata taa ya mafuta.

173 Sijui kama mmepata kujua taa ya grisi ilikuwa ni nini, ama hamjui. Unachukua mafuta ya nguruwe na kuyaweka kwenye kopo, na utumbukize kipande kidogo cha kitambaa ndani yake, kisha ukiwashe moto, nacho kitawaka.

174 Nuru hiyo, mapema hivyo asubuhi, isingeonyesha nuru ya kutosha kumfanya mama kuona nilivyokuwa, ama sura yangu. Basi walifungua dirisha hili dogo upande wa Mashariki, kwa kuwa robini fulani walikuwa wameketi vichakani huko nje, wakiimba, kwenye mapambazuko ya saa kumi na moja.

175 Basi walipofungua dirisha, Nguzo ya Moto, Nuru, iliingia kupitia dirishani, ikaja ikaning'inia juu ya kitanda hicho kidogo. Mama yangu akapiga mayowe. Mkunga alikuwapo. Hatukuwa na daktari. Naye mkunga alikuwapo. Hawakujua ilikuwa ni kitu gani.

176 Yapata majuma mawili baada ya hapo, nilibebwa nikapelekwa kwenye kanisa dogo la Kibaptisti, lililoitwa Ufalme wa Oposamu. Mhudumu alinishika mikononi mwake na kuniweka wakfu kwa Mungu.

177 Watu wa milimani hawakujua wawazie nini juu ya jambo Hilo. Hao, waliwaambia. Walidhani kwamba labda mama alikuwa amerukwa na akili, ama aliwazia tu hilo.

178 Miaka mitatu baadaye, tulikuja Indiana, naye baba akapata kazi. Alikuwa mpanda farasi, kuwafunza farasi wa maranchi na wa wakulima, na kadhalika. Alikuja huko kuwafunza farasi wengine wadogo wa kupanda, kwa ajili ya ta—tajiri mmoja jina lake O. H. Wathen, anayeishi Utica Pike. Yeye alikuwa mmilikaji mkuu wa kampuni ya Colonels, na pia Kiwanda cha pombe kali cha R. E. Wathen, na vyote huko Louisville, na O. H. na R. E. Naye baba alikuwa akiwafunza farasi wake wa matandiko. Halafu akajeruhiwa, ndipo akabadilika kuwa dereva wake binafsi.

179 Ndipo kwenye umri wa yapata miaka saba, nilikuwa nimeingia shuleni. Na alasiri moja ya Septemba . . . Ninachukia kusema hili, bali niko kwenye kizimba cha kutoa ushahidi. Baba yangu, akiwa ni Mwairishi halisi, Mkentaki mkali, alitengeneza vinywaji vyake mwenyewe. Nami nilikuwa nikiteka maji kwa ajili ya kikeneko hiki kidogo alichokuwa nacho, wala nisingeenda kuvua samaki nyuma ya kidimbwi. Nilikuwa nikilia, nikibeba maji umbali wa jumba la mji, kutoka kibandani, ambako farasi walikaa. Nami nilikuwa nikiyapeleka maji kule, kuja kubaridisha koili za kikeneko hicho kwa ajili ya usiku huo.

180 Nikaketi chini ya mti wa mpopla mweupe, huku nikilia. Maskini uso mchafu, nywele zimening'inia chini, gunzi la hindi chini ya kidole changu, kujieupusha na kisiki kikubwa, mwajua, nikiendelea namna hiyo, nimetoka shuleni. Wavulana wengine wote walikuwa huko nje kwenye kibanda cha kale cha barafu, wakivua samaki. Nilikuwa nimeketi pale, ninalia. Nikawaza, "Kwa nini inibidi kufanya hivi? Hao watoto wengine hawafanyi hivyo."

181 Na jambo ni kwamba, kelele zilikuja kwenye mti huo, kama upepo ukipinduka-pinduka, kama upepo wa kisulisuli. Ndipo nikasimama na kuangalia nyuma. Nami niko kwenye kizimba cha kutolea ushahidi, kumbukeni. Kulikuwako na Sauti iliyonena kutoka kwenye huo, iliyosema, "Kamwe usivute sigara, wala kunywa pombe, wala kuutia mwili wako unajisi. Kuna kazi utakayofanya utakapokuwa mtu mzima." Ilinishtusha nusura nife. Ndipo nikaendelea. Mambo yakaanza kutukia. Mambo yakaaza kutabiriwa na kutukia. Na sasa, nilipokuwa mvulana mdogo, basi, yapata umri wa miaka saba.

182 Halafu, yapata miaka kumi na saba baada ya hayo, nilikuwa, nilikuwa nimefanyika mhudumu, mhubiri Mbaptisti, wa Kanisa la Kimishenari la Baptisti. Dk. Roy E. Davis aliniweka wakfu kama mmoja wa wachungaji wa mahali hapo, akanipa haki wakati huo, za taifa, kufungisha ndoa, kuzika, kubatiza, na kadhalika. Kisha Kanisa la Kimishenari la Baptisi likateketea, ambamo nilikuwa mchungaji msaidizi, wakati huo. Naye Bw. Davis akarudi Texas, ambaye alikuwa ametoka kwenye milima ya Davis, na—na huko chini karibu na Van Horn, Texas. Huko ndiko walikotoka. Na kwa hiyo, wakati alipokuwa ameondoka, nilianza kuchukua mamlaka juu ya kusanyiko. Nikapata hema, na kuanza kuhubiri mjini, na ni mhubiri mvulana tu.

183 Nami nilikuwa na ibada ya ubatizo huko mtoni, mwaka wa 1933, katikati ya Juni, mnamo tarehe kumi na sita au kumi na nane Juni. Nami nikisimama huko nje, kulikuwa kumekuwa joto sana, kwa majuma kadhaa. Hakukuwako na mvua kwa majuma mawili ama matatu, nayo nchi ilikuwa ikiungua, karibu iungue. Basi kulikuwako, nadhani, yapata watu elfu saba ama elfu nane ufukoni. Ndipo nikaingia majini, nikiwa na mtaradhiwa wangu wa kumi na saba, kumbatiza. Basi nilipombatiza, nilipoanza kumbatiza, nilisema, "Ninapokubatiza kwa maji, naomba Bwana Yesu . . . "

184 Niliposema hivyo, kitu Fulani kilinigusa na kusema, "Angalia juu." Basi nilipogeuka kuangalia, baada ya Hiyo kusema mara ya tatu, mahali pa karibu futi kumi na tano mraba palikuwa pakivurugika juu chini katika anga hizo za shaba. Na kutoka huko ikashuka Nguzo ile ile ya Moto iliyoingia wakati nilipokuwa mtoto mchanga, iliyosema nami katika kijiti kilichowaka moto, ama kichaka kule nyuma siku hiyo, na

kuingia kwenye kichaka kile, kisha ikaja na kuning'inia ambapo maelfu ya watu walikuwa.

185 Magazeti yaliyatangaza kote nchini, hadi Kanada. Tuna nakala zilizokatwa. "Nuru ya ajabu yatokea juu ya mhudumu wa Kibaptisti wakati akihubiri, ama akibatiza."

186 Ndipo Sauti hiyo ikashuka na kusema, "Kama Yohana Mbatizaji alivyotumwa, kutangulia kuja kwa kwanza kwa Kristo, vivyo hivyo Ujumbe wako utatangulia Kuja kwa pili kwa Kristo."

187 Ingewezaje kuwa hivyo? Ingewezaje kuwa hivyo? Ilionekana kana kwamba isingewezekana. Ndipo wakati iliponena, siku chache kutoka hapo, na kusema. Ndipo nikaanza kuona maono haya na mambo ambayo daima yalitukia. Yangenishtusha.

188 Ndugu zangu waliniambia, kasema, "Hayo ni ya ibilisi." Ndugu zangu Wabaptisti walisema, "Hayo ni ya ibilisi."

189 Nilisema, "Unajua, nitakuwa tu nimesimama, na," nikasema, "jambo la kwanza mwajua, itaingia katika namna fulani ya mpagao, kama, au kitu fulani." Nikasema, "Mimi huona mambo ambayo sikuzote yanatukia. Yeye aliniambia, miaka ishirini na miwili kabla lile daraja halijavuka ng'ambo ya pili pale, kwamba litafika umbali gani ng'ambo ya pili, wakati litakapojengwa, na ni watu wangapi watapoteza maisha yao. Nalo ni kamilifu, kila wakati."

Halafu baadhi yao wakasema, "Huyo ni ibilisi."

190 Ndipo nikaondoka, na kuanza kulia na kuomba, usiku mmoja. Nikasema, "Bwana Yesu, Wewe unaujua moyo wangu. Ninakupenda. Acha nife. Usiache niwe na ninii yoyote . . . ibilisi kuwa na uhusiano wowote nami. Afadhali nife kuliko kuwa shahidi Wako wa uongo."

191 Na ilikuwa ni kwenye wakati huo ambapo Nuru hii ilirudi tena na kunionyesha Maandiko, kwamba katika siku hii jambo hili linapaswa kutukia. Hili hapa moja kwa moja katika Maandiko sasa. Imekuwa miaka thelathini na mitatu tangu wakati huo, bali mimi ni shahidi ya kwamba ni Kweli. Mimi ni shahidi wa mambo haya kwamba ni Kweli.

192 Na hebu ni—nimhamasishe mwendesha mashtaka huyu aliye kipofu Kimaandiko. Sasa, hili litasikika la kidhihaka. Huyu mwendesha mashtaka, ni kipofu Kimaandiko. Kwamba, katika Kitabu cha Luka Mtakatifu, mlango wa 17 na kifungu cha 30, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma."

193 Sasa, mnataka kujua ambapo huyu ni mwanadamu, kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Mnataka kujua yalipo makovu ya misumari na majeraha, na kadhalika? Mnafiki yeyote anaweza kufanya hivyo.

194 Uhai wa Kristo unarudi katika mfano wa Roho Mtakatifu, sio kovu la msumari. Mwi—mwili wa kawaida umeketi mkono

wa kuume wa Mungu, kufanya uombezi, bali Roho Mtakatifu amekuja kuendeleza kazi Yake. Nawatakeni mjue, katika Yohana Mtakatifu 14:5, Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Ninawatakeni pia mjue ya kwamba Yohana, wa 14 . . . ama mlango wa 15 unasema, ya kwamba, "Mimi Ndimi Mzabibu; ninyi ni matawi." Nayo matawi yanawezaje kuzaa uhai wa aina nyingine yoyote ama tunda mbali na lile lililokuwa kwenye huo mzabibu?

195 Ninyi watu mnawezaje kusema ya kwamba wakati wa kimitume ulikwisha? Mnalipata wapi? Mzabibu unawezaje kutoka na kuzaa, leo hii, unawezaje kutoka nje na kuzaa chungwa, na siku *hii* uzae boga? Ingebidi ubadilishe uhai wake. Na katika Malaki mlango wa 3, Mungu alisema, "Mimi ni Mungu, na sina kigeugeu." Kile alichokuwa wakati huo, ndicho alicho leo. Naye sikuzote alikuwa hivyo na daima atakuwa hivyo.

196 Ninataka kuwaita, usikivu wenu, kwamba mwendesha mashtaka anajaribu kuwaambia ya kwamba Yeye—Yeye alisema, "Nilikuwa" ama "Nitakuwa," bali ni uongo. Alisema, "Mimi ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Huyu mwendesha mashtaka analifasiri Neno vibaya.

197 Wakati Yesu alipowaagiza wanafunzi Wake waende kote ulimwenguni, katika Marko 16 hapa, na kuihubiri Injili kwa kila kiumbe. Umbali gani? "Ulimwenguni kote," kamwe haijaufikia. "Kila kiumbe," kamwe haijawafikia. "Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka. Asiyeamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana nao hata mwisho wa ulimwengu. Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya."

198 Ninawatakeni mjue pia ya kwamba Petro, kwenye Siku ya Pentekoste, ambaye alikuwa na funguo za Ufalme, wakati aliposimama katika Matendo 2:38. Alisema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."

199 Wakati wa mitume ulikoma lini? Hilo hapo agizo, "Ulimwenguni kote, kila kiumbe, na kila aaminiye." Ninaitaka mahakama kufahamu hilo, kwamba hiyo ni ahadi ya Mungu.

200 Ninawatakeni mfahamu pia, mfasiri huyu kipofu kwa watu hayafahamu Maandiko. Yeye alisema, hapa katika Marko, m—mlango wa 17 na kifungu cha 30, alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma." Sasa rudini nyuma. Yesu alikuwa akirejea kwenye Mwanzo ule ule tunaorejea sisi. "Katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Sasa rudini nyuma mwangalie ilivyokuwa

katika siku za Sodoma, ndipo mwone mahali tulipo na mwone kinachopaswa kutukia sasa. Katika siku za Sodoma, wakati . . .

201 Ibrahimu, ambaye alikuwa ni mfano, yeye . . . Sisi, tukiwa tu tumekufa katika Kristo, tunachukua uzao wa Ibrahimu, na ni warithi pamoja naye sawasawa na ahadi. Yeyote wenu mahakamani, alasiri ya leo, anajua hilo.

202 Mwangalieni Ibrahimu. Alipokea kila namna ya ishara, kila kitu, kutoka kwa Mungu wa kimbinguni katika mfano wa Nuru, akipitia katikati ya sadaka. Alimpokea katika sauti, na kadhalika. Lakini ishara ya mwisho ambayo Ibrahimu aliipokea juu ya Mlima kutoka Sodoma, kabla tu ya kuangamizwa ulimwengu wa Mataifa, ilikuwa ni Mungu Mwenyewe katika umbo la Mwanadamu. Mnafahamu, enyi mahakama? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kulikuwako na Wajumbe watatu waliomjia. Wajumbe watatu, naye akatoka kwenda kuwalaki.

203 Wawili wao, Oral Roberts wa kisasa na Billy Graham, wanashuka kwenda Sodoma na kuihubiri Injili, nao wakawapofusha kwa Injili yao.

204 Bali Huyu aliyeketi huko nyuma, aliyekula nyama ya ndama, akanywa maziwa kutoka kwa ng'ombe, na kula mkate, na Ibrahimu akaitawadha miguu Yake. Basi aliketi pale, Mwanadamu. Na akasema . . .

205 Sasa, kumbukeni, jina lake lilikuwa Abramu, siku moja kabla ya hapo, nalo lilikuwa limebadilishwa likawa Ibrahimu. Na Sarai lilikuwa limebadilishwa likawa Sara. Basi mwangalieni, yale anayosema, "Yu wapi Sara, mkeo?" S-a-r-a. "Ibrahimu," I-b-r-a-h-i-m-u, "yu wapi Sara, mkeo?"

206 Akasema, "Yumo hemani nyuma Yako." Hakuwa ametoka, kama vile wanawake siku hizi wanavyofanya, ambao inawabidi kujionyesha. Lakini, yeye, alikuwa hemani huko nyuma.

Akasema, "Nitakurudia majira kama haya mwakani."

207 Ndipo Sara akashuku moyoni mwake, na kusema moyoni mwake, "Mambo haya hayawezekani," maana, mnaona, uhusiano wa kifamilia ulikuwa mbali nao. Alikuwa na umri wa miaka mia moja, naye mke alikuwa na tisini. Kasema, "Ati mimi nipate raha na bwana wangu, naye ni mzee, pia, huko nje? Inawezekanaje?"

208 Naye Mtu huyu, mgongo Wake ukiwa umegeuzwa kuelekea hemani, akasema, "Kwa nini Sara akashuku, akisema, 'Mambo haya hayawezekani'?"

209 Naye Ibrahimu alimwita "Elohimu." Kama mtu yeyote anajua *Elohimu* linamaanisha nini, "ajitoshelezaye kwa yote." Mwenyezi Mungu Mwenyewe akidhihirishwa katika mwili. Ibrahimu alimwitaje hivyo? Kwa maana aliona kuwa Mtu huyo alikuwa ni Neno.

210 Sasa, Waebrania, mlango wa 4 na kifungu cha 12, inasema ya kwamba Neno la Mungu lina ukali kuliko upanga ukatao kuwili, Tambuzi la mawazo na makusudi ya moyo. Na Yesu alipokuja na kufanya mwujiza huo, kwa kuyatambua mawazo yao yaliyokuwa moyoni mwao, walimwita Belizebuli.

211 Lakini Neno katika manabii hao daima liliweza kutabiri na kutambua. Hilo ndilo Neno la siku hiyo. Hilo ndilo lililowatambulisha kama manabii. Basi kumbukeni, Yeye aliahidi ya kwamba ulimwengu ungekuwa katika hali hiyo, nao ungepokea ishara hiyo tena kabla ya Kuja Kwake. Sasa angalieni katika Luka 17 hapa, Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu, wakati Mwana wa Adamu anapofunuliwa."

212 Mwaweza kunivumilia kwa dakika nyingine, mniruhusu niwafungulie jambo lingine hapa, kwa dakika moja tu, enyi mahakama? Mtaruhusu jambo hili, kwa kuwa mimi ni shahidi?

213 Hivi mliona hapa? Kamwe hakusema, "Wakati anapofunuliwa Mwana wa *Mungu*." Alisema, "Mwana wa Adamu." Yesu alikuja na sifa tatu: Mwana wa Adamu, Mwana wa Daudi, Mwana wa Mungu, wote Mtu yeye yule.

214 Hiyo ni kama tu utatu: Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Sio Miungu watatu! Mtu mmoja; sifa tatu za Mungu.

215 Sasa, mnaona, ni kama tu vile mimi nilivyo watu watatu. Mimi kwa mke wangu ni mume. Mimi kwa binti yangu, anayeketi hapa, ni baba. Na mjukuu wangu, anayeketi pale, mimi ni babu. Sasa, mke wangu ana madai juu yangu tu kama mumewe. Naye binti yangu hapa hawezi kusema, "mume," kwa kuwa yeye ni mtoto wangu. Mjukuu wangu hawezi kuniita "baba." Kweli. Hana madai juu yangu kama baba. Huenda akaniita hivyo, bali sivyo ilivyo. Yeye ni mjukuu wangu. Hata hivyo, mimi ni mtu yule yule.

216 Ni Mungu akijifunua Mwenyewe, akijishusha chini, apate kuwa. . . Yeye alikuwa huko juu, katika Nguzo ya Moto. Ndipo akadhihirishwa katika Mwanawe, Yesu Kristo. Na sasa amefunuliwa kwetu, kwa Roho Mtakatifu. Angalieni, wakati alipokuja.

217 Mnajua kile "Mwana wa Adamu" linamaanisha? Angalieni katika Ezekieli, mlango wa 2, nanyi mtaona, Ezekieli 2:1. Yehova Mwenyewe alimwita Ezekieli, nabii, "mwana wa Adamu." Aliwaita manabii wote, "mwana wa Adamu."

218 Basi ni kwa nini Yesu alijiita Mwenyewe Mwana wa Adamu? Kwa sababu ilimbidi kuja jinsi manabii walivyosema angekuja. Musa, katika Kumbukumbu la Torati 18:15, alisema, "Bwana Mungu wako atakuondokeshea nabii kama nilivyo mimi." Naye alikuja kujifunua Mwenyewe kwa uzao wa kimwili wa Ibrahimu, kama Mwana wa Adamu. Nao wakaiita kazi ya ibilisi.

219 Vivyo hivyo na Uzao wa kifalme! Hilo linasikika kuwa kali, bali ni sahihishi, na ni upendo. Uzao wa kifalme siku hizi umefanya jambo lile lile; kujaribu kuiita "kuwasiliana kimawazo, ama ibilisi fulani." Ni Mwana wa Adamu, Kristo.

220 Huyo alikuwa ni Kristo ndani ya Ezekieli; Kristo ndani ya Musa; Kristo ndani ya Daudi. Ilikuwa ni Yesu, yeye yule jana, leo, na hata milele. Kitu gani? Neno likidhihirishwa na hawa manabii.

221 Lisikilizeni, enyi mahakama, kabla hamjatoa uamuzi wenu. Neno humjia nabii. Yesu alisema ya kwamba torati yenu inasema ya kwamba ninii yenu. . . ya kwamba hao waliojiliwa na Neno la Bwana ni miungu. Naye Yesu alikubali kwamba walikuwa miungu. Alisema, "Basi, kama mnaweza kuwaita na kuwatambua, torati yenu, kama miungu, ambao walijiliwa na Neno la Bwana, manabii, mtanihukumuje ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu?" Wakati, Yeye Ndiye Neno lililothibitishwa la wakati huo. Walisema kwamba waliwaamini manabii, nalo hili hapa lile Neno katika utimilifu. Na hata hivyo hawakuliamini bado, kwa kuwa walikuwa na kanuni zao za imani na mapokeo yao.

222 Angalieni sasa, enyi mahakama, kabla hamjatoa uamuzi wenu. Hebu twende mbele kidogo. Angalieni. Mwana wa Adamu, walimwita ibilisi. Bali walitaka kumfanya mfalme, mwajua, kwa nguvu.

223 Angalieni, wakati kipofu Bartimayo alipomkimbilia, alisema, "Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu," yeye alipata alichoomba.

224 Bali wakati yule mwanamke Msirofoinike, Myunani, Mmataifa, alipomfuata mbio na kusema, "Ewe Mwana wa Daudi," Yeye hata hakukiinua kichwa Chake. Yeye hakuwa na madai juu Yake kama Mwana wa Daudi. Hakuwa Mwana wa Daudi kwake. Bali aliposema, "Mwana wa Mungu" ama "Bwana," ambalo ni Mwana wa Mungu, alipata alichoomba. Mnaona? Mataifa hawana dai juu Yake kama Mwana wa Daudi. Yeye alikuwa ni Mfalme. Yeye ni Bwana, kwetu.

225 Na hapo alipojifunua Mwenyewe kama Mwana wa Adamu, kama vile Maandiko yalivyosema angekuwa. "La, bwana." Walimkataa. "Yeye hakuwa nabii." Wasingeweza kuamini Hilo. Hawakuwa wamepata mmoja kwa mamia ya miaka, nao wasingemwamini kuwa nabii.

226 Wakati alipomwambia maskini mwanamke yule kwamba alikuwa na wanaume wangapi, naye akiwa katika hali hiyo, alikuwa amekusudiwa Uzima. Akasema, "Bwana, naona kwamba Wewe u nabii. Najua wakati atakapokuja Masihi. Hatujakuwa na nabii kwa mamia ya miaka. Bali najua, atakapokuja, hiyo ndiyo ishara atakayofanya, maana Yeye atakuwa ni Neno. Anajua yaliyo moyoni mwangu."

227 Akasema, “Mimi Ndimi ninayesema na wewe.” Nao ushuhuda wake ukaufanya mji mzima kumjia Kristo. Kweli. Wote waliamini.

228 Sasa, angalia, kama Mwana wa Daudi, Yeye alikuwa pamoja na Wayahudi. Bali Mwana wa Mungu . . . Sasa angalieni. Mwana wa Adamu, nabii. Mnaona? Mwana wa Daudi, mfalme. Hawakumtambua kama nabii. Walitaka kumfanya mfalme. Walitaka kukombolewa watoke chini ya Himaya ya Kirumi.

229 Lakini basi katika wakati wa kanisa, Yeye anaitwa Mwana wa Mungu. Sasa, mtu yeyote anajua kwamba Mungu ni Roho. Je! hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Naye Roho Mtakatifu ni Mwana wa Mungu. Ni wa kimbinguni. Mwana wa Adamu alikuwa ni nabii, mwanadamu; Daudi alikuwa mfalme; lakini Mungu ni Roho. Na katika wakati wa kanisa, Yeye anafunuliwa kama Mwana wa Mungu. Tunaamini hivyo. Usipoamini Yeye ni Mwana wa Mungu, umepotea. Yeye ni Mwana wa Mungu kwa wakati wa kanisa.

230 Bali nishuhudieni. Wakati wa saba wa kanisa, ambao ni wakati wa kanisa la Laodikia! Vema, tungekubali ya kwamba huu ni wakati wa Laodikia? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kumbukeni, Yeye, Neno, aliondolewa kanisani. Hiyo ni kweli? [“Amina.”] Aliondolewa kanisani! Naye alikuwa nje, akijaribu kurudi ndani, “Nasimama na kubisha mlangoni.” [Ndugu Branham anagonga mara tatu mimbarani.] “Nawe wasema kwamba, ‘Mimi ni tajiri, wala sina haja na kitu.’ Wala hujui ya kwamba wewe ni mwenye mashaka, kipofu, uchi, mnyonge, wala hujui.” Alikuwa nje, lile Neno.

231 Ni kitu gani? Mapokeo yetu. Mapokeo yetu ya Kimethodisti, Kibaptisti, Kipresbiteri, Kipentekoste yamelikataa Neno, wala hawezi kupata ushirikiano wowote popote. Kila mtu ni “achana Nalo,” nao wanataka kuliita pepo mchafu.

232 Basi mnafahamu ya kwamba Yesu alisema, katika siku za mwisho kabla ya kuja kwa wakati wa mwisho, ya kwamba Yeye angefunuliwa tena kama “Mwana wa Adamu,” sio “Mwana wa Mungu”? Na hiyo inatimiza Malaki 4 na ahadi hizi zingine zote za Ibrahimu, ile ishara ya mwisho aliyopokea Ibrahimu. Alikuwa akimngojea mwana ajaye, nayo ishara ya mwisho aliyoipokea, ilikuwa ni Mungu aliyefunuliwa katika mwili wa mwanadamu. Naye Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu huko, Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.”

233 Sasa, samahani, nipate kutoa tamshi dogo la kilindi hapa. Ninataka kuwaulizeni nyinyi wanathiolojia jambo fulani. Tafuteni kote katika Maandiko, katika historia ya Biblia. Kama vile mmekuwa mkiniambia juma hili, mlikuwa ninii—mlikuwa watu wanaoyasoma Maandiko. Na pia kwamba mlikuwa . . . kwamba wakati wa kimitume umekwisha, na—na kwamba—

kwamba mliijua historia yote ya kanisa. Ninataka mlitafakari hili. Mungu na anisamehe kwa kulichambua hili, kama si halali kufanya hivyo.

234 Ulimwengu umekaa katika wakati wake kabisa. Ulimwengu kamwe haujawahi kuwa katika hali ya namna hii, kama katika hali ya Sodoma. Juma lililopita, huko Florida, jimbo la Florida, asilimia sitini na kitu ya waalimu wa shule waliondolewa shuleni, kwa sababu ya ulawiti. Uliongezeka asilimia arobaini na kitu, huko Kalifornia, katika mwaka uliopita; ulawiti. Shule, seminari, kila kitu kimejaa huo. Nao umekaa mahali ulipokuwa hasa katika siku za Sodoma. Mungu atawajibika, asipoliadhibu taifa hili pamoja na ulimwengu huu kwa ajili ya dhambi zake, Yeye atawajibika kiadilifu kuuinua Sodoma na—na Gomora na kuomba msamaha kwa ajili ya kuiteketeza. Angalieni saa tunayoishi.

Wazieni sasa, kwa dakika moja, enyi mahakama, kabla hamjafanya uamuzi wenu.

235 Sasa, Yesu kamwe hakusema, "Katika siku atakapofunuliwa Mwana wa Mungu." Alifunuliwa katika wakati wa kanisa. Lakini kanisa limemtoa nje.

236 Basi, Yeye atafunuliwa kama Mwana wa Adamu, "Wakati Mwana wa Adamu anapofunuliwa," Mungu akidhihirishwa miongoni mwa wanadamu, kama ilivyokuwa wakati huo, Mwana wa Adamu, nabii.

237 Malaki 4 pameahidiwa, mwo—mwonaji kuja na sauti. Sio Malaki 3 sasa, "Kumtuma mjumbe Wangu." Malaki 4 sasa. Msivichanganyishe. Maana, mkivichanganya, mtalikosa. Malaki 4 haikuwa ni Malaki 3, "Namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu." Lakini, Malaki 4, wakati mjumbe huyu atakapokuja, ulimwengu utateketezwa, kisha ule Utawala wa Miaka Elfu unaanza. "Waovu wanachomwa moto, wakawa majivu, nao wenye haki wanatembea juu ya majivu yao." Hilo halikutukia katika siku za Yohana. Mnaona? Malaki 4! Pia angalieni, kunapaswa kuwepo na ishara, na ishara hiyo haina budi kuwa ni ishara ya Kimaandiko.

238 Yesu alisema, "Nimetoka kwa Mungu. Naenda kwa Mungu." Yeye alikuwa ile Nguzo ya Moto iliyokuwa kwenye kichaka kilichowaka moto.

239 Walisimama pale siku moja na kusema, "Wewe ni Mtu asiyepata bado miaka hamsini." Huenda alionekana mzee kidogo kuliko alivyokuwa hasa. Huduma Yake ilikuwa inalemea. Nayo Biblia ilisema hamna uzuri hata tumtamani, na labda ni maskini Jamaa mdogo. Yeye alisema, "Mnasema . . . Hujapata bado miaka hamsini. Vema, hujapata bado zaidi ya miaka hamsini, Nawe wasema ulimwona Ibrahimu?"

240 Akasema, “Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.” Akasema, “Nimetoka kwa Mungu. Nilikuwa ile Nguzo ya Moto nyikani. Nimetoka kwa Mungu.”

241 Alifanyika mwili, Mwana wa Mungu. Mungu alimtia bikira uvuli, akaumba seli ya Damu ambayo ilimzaa Mwanawe. Ambaye, Mungu alifanya maskani katika huyo Mwana. “Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.”

“Nami naenda kwa Mungu,” baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka.

242 Sauli alikuwa akienda zake Dameski, naye akapigwa na Nuru akaanguka chini, ile Nguzo ya Moto. Mnafikiri Myahudi huyo angeita chochote, na—namna fulani ya mazingaombwe, “Bwana”? Alipoangalia juu na kuiona ile Nguzo ya Moto, alijua ya kwamba hiyo ndiyo yeye, baba zake walikuwa wameifuata, waliyoifuata kutoka Misri. Akasema, “Bwana, U nani Wewe?”

243 Naye akasema, “Mimi ni Yesu.” Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

244 Nayo sauti ya Kimaandiko iliyonena katika kile kichaka cha Musa, naye Musa akashikilia kusimama juu yake.

245 Vivyo hivyo na ile sauti ya Kimaandiko iliyonena kichakani, kwenye umri wa miaka saba. Ningali ninasimama na kusema ni Kweli. Kwa maana, Musa aliliona lile Neno, ilibidi litimie. Ninaona Neno hili halina budi kutimia. “Mwana wa Adamu hana budi kufunuliwa,” vile vile lilivyosema hasa. Angalieni, liliahidi hilo. Sio Mwana wa Mungu; Mwana wa Adamu! Mnaona? Mwana wa Adamu, Mwana wa Daudi, na Mwana wa Mungu.

246 Lakini baada ya siku za wakati wa kanisa, wakati ametolewa nje, ndipo Yeye anajifunua tena kama Mwana wa Adamu. Maana, “Sisi tukiwa tumekufa katika Kristo, tunachukua Uzao wa Ibrahimu.” Nasi ni Uzao Wake wa kifalme. Ni wangapi wanakubali hilo, ya kwamba Kanisa ni Uzao Wake wa Kifalme? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema, mnaona, kile alichomfanyia Ibrahimu, Yeye anafanya jambo lile lile.

247 Sasa samahani jambo hili. Sasa, ninyi jamaa mnaosema mnajua historia vizuri sana, niambieni ni wakati gani, katika historia ya kanisa, kumepata kuwako na kiongozi ambaye alitoka akawaendea ninyi huko nje, pamoja nanyi Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Lutheri, chochote mnachoweza kuwa? Ni lini paliwahi kutokea mtu aliyetumwa kwenu, ambaye jina lake linaishia kwa h-a-m, hadi sasa, G-r-a-h-a-m? Mlikuwa na akina Sankey, Moody, Finney, Knox, Calvin, bali kamwe si h-a-m, kama vile Abraham. Nalo G-r-a-h-a-m ni herufi sita pekee.

A-b-r-a-h-a-m ni herufi saba, Neno la Mungu, lililokamilika.

248 Sasa, kumbukeni, mtu huyu aliyekuwa katika siku za Ibrahimu. Sasa, Ibrahimu alikuwa, ninii yake, alikuwa mteule. Yeye hakuwa huko Sodoma. Aliitwa atoke Sodoma. Yule Mjumbe aliyemtembelea hakwenda Sodoma.

Lakini, wale walioshuka kwenda Sodoma, angalieni yale waliyofanya.

249 Angalieni yale Huyu aliyolifanyia kanisa teule. Naye Yesu alielekeza usikivu wenu kwa jambo lilo hilo, litakalotukia katika siku za mwisho, "hapo Mwana wa Adamu atakapojifunua Mwenyewe katika mwili wa binadamu," Neno likiifahamu siri ya moyo. Kama lilivyosema, "Lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, na Huyatambua mawazo na makusudi ya moyo." Kama vile manabii wote walivyofanya. Kama vile Yesu alivyofanya, Mwenyewe, alivyoitwa Beelizebuli. Na kukataliwa hapa, tena, katika siku za mwisho.

250 Nashangaa kama huyo mfasiri kipofu alipata kuwazia jambo hilo? Nashangaa kama atawahi kutambua ya kwamba Maandiko haya yaliyotabiriwa kwa ajili ya siku hii hayana budi kutimia? Jinsi labda...Mnaamini haina budi kuwa ni wakati huu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Neno la Mungu, ingawa litakawia! Hata hivyo mambo haya yote, nyakati hizi za kanisa zilipita, na imekuwa ni mamia ya miaka tangu tulipokuwa nalo, bali limeahidiwa kuwa hapa.

251 Yeye amejifunua Mwenyewe kama Mwana wa Mungu, Mwana wa Mungu, kubatizwa kwa Roho Mtakatifu. Kanisa la Kipentekoste na makanisa kotekote, yamezishusha ishara, maajabu, miujiza kama alivyofanya. Wamemwona Mungu katika maono makuu na kila kitu.

252 Bali kamwe kanisa halijapata kumwona Mwana wa Mungu akidhihirishwa katika mwili wa mwanadamu, ambaye angeyatambua mawazo yaliyo moyoni, mpaka wakati huu. Na huo ndio wakati ambapo Sodoma itateketezwa na mwana aliyeahidiwa arudi. Nashangaa kama mfasiri huyo kipofu wa Maandiko alipata kuwazia hilo? Ninaitaka mahakama kukumbuka hilo. Kumbukeni, haidhuru ni kirefu vipi, haidhuru litachelewa muda gani, hata hivyo halina budi kutukia. Litatukia.

253 Mashahidi hawa wanashuhudia, hakika wameshuhudia Ukweli, kwamba ndivyo ilivyo. Mungu alisema, "Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya."

254 Lakini ulimwengu wa nje unataka uamini, mara unapoiweka mikono yako juu ya mtu, huna budi...na miguu iliyolemaa haina budi kunyoka, na huna budi kuruka-ruka. Kamwe Yeye hakusema hivyo. Hakuahidi hilo.

255 Alisema, "Maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa huyo, Naye Mungu atamwinua." Kamwe hakusema ni wakati gani. "Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya."

Kamwe hakusema ni lini. Alisema, "Mwombapo, aminini kwamba mnapokea, nanyi mtapewa." Hakusema lini.

256 Sasa, kama sisi ni waaminio halisi, wa kweli, wakati Maandiko haya yanapodhihirishwa kwetu, hakuna kitu kinachoweza kutwambia vinginevyo. Hakuna kitu kinachoweza kusema ya kwamba ni uongo; ni wangapi wangeweza kuinuka, ni makafiri wangapi, ni wasioamini wangapi, ni wangapi wangeweza kuelezea *hili*, *lile*, ama *lingenelo*. Mungu hudumisha Neno Lake. Nayo Marko 16 imevuviwa tu sawasawa na Yohana 3:16. Kitu hicho chote ni Neno la Mungu. Kila Neno Lake limevuviwa. Lote ni Mungu, kama ukilisoma tu jinsi linavyosema.

257 Nataka kulitazamisha kanisa taratibu ya siku, wachunguze. Kabla ya kuita chochote ibilisi, afadhali ukumbuke, ahadi ya hili inapaswa kuwa kwenye siku hii. Mnaona? Kumbukeni hilo. Maana, neno moja dhidi ya Roho Mtakatifu halisamehewi katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao. Nanyi mnamwona Roho Mtakatifu Mwenyewe akidhihirishwa, akifanya jambo lile lile.

258 Ninamwangalia maskini mwanamke anayeketi hapa mbele yangu. Nafikiri ni Mpresbiteri. Sijakosea. Alikuwa nyumbani kwangu, si muda mrefu uliopita. Alikuwa aishi mpaka Jumatano, kansa; ameketi chumbani. Ilitokea tu nilimwona ameketi karibu na rafiki yangu. Naye alikuwa amepewa kuishi mpaka Jumatano, na madaktari wa mjini. Wameshangaa sasa. Huyu hapa ameketi usiku wa leo, akionekana mzima na mwenye afya, na angali anaishi. Unashukuru kwa ajili ya jambo hilo, sivyo, dada? Inua mkono wako, kama hiyo ni kweli. Mwangalieni ameketi papa hapa. Mnaona? Akifa, na amepewa hadi Jumatano, yapata miezi kadha iliyopita. Na sasa madaktari wameshangaa sana, kuliwazia. Kilichotukia kilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI. Maneno Yake yangali ni kweli.

259 Wakati, Andiko hili linasema hapa, kwamba, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya, kama utaamini. Ishara hizi zitafuatana na mwaminio." Watapata afya. Hakusema ni lini. Na endapo wewe ni mwaminio halisi, hakuna kitu kingaliweza kukutenga na hilo.

260 Usikilizeni ushuhuda wa Ibrahimu. Sikilizeni shuhuda zingine zao. Ni mamia wangapi ningaliweza kuita jukwaani leo, na kuwaonyesha ya kwamba Mungu hudumisha Neno Lake, haidhuru, kama utaliamini na kusimama pale, na kujua moyoni mwako kuwa itatendeka.

261 Wakati, maskini mama huyu, tunayemrejea. Sasa, mtu fulani alikuwa akiniambia, dakika chache zilizopita, samahani, alikuwa akiniambia dakika chache zilizopita, akipitia kwenye mstari wa chakula cha jioni pale, kasema, "Ndugu Branham,

hivi humkumbuki maskini mama huyu hapa, maombi yako ya imani kwake si muda mrefu uliopita? Yeye, miaka kadhaa iliyopita, alikuwa akifa kwa kansa." Huyo mwanamke yupo? Mtu fulani alinionyesha huyo. Inua mkono wako, kama umeketi hapa mahali fulani. Mwanamke mdogo akija kupitia mstarini, mwanamume fulani, ndugu mwenye mvi, alikuwa akinionyesha huyo, akasema alikuwa akifa kwa kansa. Naye huyu hapa anaishi sasa. Je! mama huyo yumo humu chumbani sasa? Alikuwa kwenye chumba cha chakula cha jioni, muda mfupi uliopita. Nilionyeshwa *pale*. Naam. Naam. Yule pale Bibi Waldrop kule nyuma, aliyekaa...na akafa, mstarini, miaka kumi na mitano iliyopita, miaka kumi na saba iliyopita, pamoja na daktari wake aliyekuwa na—aliyekuwa na eksi-rei pale, ambapo kansa ilikuwa imeula moyo wake kabisa. Bali ilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI.

262 Acheni wakosoaji wainuke na kusema watakalo kusema. Mimi ni shahidi kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele. Alichokuwa wakati huo, ndicho alicho leo. Yeye si "Niliyekuwa," "Nitakuwa." Yuko sasa, wakati uliopo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Naye Yesu na Neno Lake ni kitu kile kile. Naye ni Neno. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

263 Yeye alisema nini? "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu wagonjwa, watapata afya."

264 Kabla hatujaiambia mahakama jambo hili, ninyi ndio baraza la wazee wa mahakama. Mmeisikia kesi hii. Tungeweza kuwaita mashahidi wangapi? Haidhuru mwe—mwendesha mashtaka angeweza kuwaita mashahidi wengine wangapi, Maneno haya yanashuhudia dhidi yake. Yeye anayafasiri vibaya Maandiko. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Maneno haya ni ya kweli? Ni wangapi walio waaminio? Inua mkono wako. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema. Biblia ilisema jambo hili, "Maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa. Mungu atamwinua. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya."

265 Sasa angalieni, kila mmoja wenu. Kupitia ujumbe huu mdogo uliovunjika-vunjika, mmefanya uamuzi fulani. Ndani ya moyo wako, umefanya uamuzi wako, maana hilo ni baraza la wazee wa mahakama. Basi jinsi utakavyotenda baada ya hapa, hiyo itathibitisha jinsi uamuzi wako ulivyo. Unaona? Jinsi utakavyoishi baada ya hapa itathibitisha tu kuwa uamuzi wako ni gani. Sasa, kama ukitoka na kusema, "Vema, mimi ni mgonjwa tu kama nilivyokuwa nilipoingia," hapo inaonyesha tu aina ya uamuzi uliofanya humu mahakamani alasiri ya leo.

266 Nafikiri kesi ambayo amefanyiwa ni ya haki, ameletwa kama Neno. Amethibitishwa kama Neno. Ametambulishwa kama Neno. Na kama nikifa usiku wa leo, Maneno ambayo nimesema

ni ya kweli. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ulimwengu unajua hilo. Ulimwengu wa sayansi unajua hilo. Nguzo ile ile ya Moto, Malaika yule yule wa Bwana! Ni wangapi wameiona picha Yake? Inaning'inia Washington D.C., Kiumbe cha pekee cha kimbinguni kilichopata kupigwa picha. Kama nikifa usiku wa leo, nisiweze kuwaona tena, yale ambayo nimesema ni Kweli. Naye Mungu amelishuhudia, kwamba ni Kweli. Na haya hapa Maandiko, yanayosema inapaswa kuwa ni wakati huu. Basi iite ibilisi ukitaka. Hiyo itakuwa ni kati yako na Mungu. Unaona?

267 Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Naye anajitambulisha kama alivyoahidi. Tungeweza kusema mengi zaidi. Katika siku hizi za mwisho, kama Mwana wa Adamu, akijitambulisha miongoni mwa watu Wake, katika umbo la watu Wake. Mnaona? Sio Mwana wa Mungu, sio Mwana wa Daudi, bali Mwana wa Adamu. Mwana wa Mungu alikuwa ni wa kimbinguni.

268 Kama vile Ibrahimu, aliona sauti, na kusikia mambo, na kuona nuru, na kadhalika. Bali kabla tu ya kuja kwa mwana aliyeahidiwa, Mungu alijifunua Mwenyewe kama Mwanadamu, katika mwili wa mwanadamu, na akayasoma mawazo yaliyokuwa katika moyo wa Sara, chumbani nyuma Yake. Ni wangapi wanaosema, wanaojua hayo ni Maandiko? [Kusanyiko linasema, "Amina."—mh] . . .? . . .

269 Naye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Mungu atakapokuja, wakati Mwana wa Adamu atakapokuwa akifunuliwa." "Mwana wa Adamu akifunuliwa," sio Mwana wa Mungu katika wakati wa kanisa. Ametolewa nje ya huo. Sasa Yeye ni Mwana wa Adamu akijifunua Mwenyewe. Neno linafanyika mwili miongoni mwetu.

270 Loo, rafiki yangu, yafungue macho yako, enyi mahakama, kabla hujatoa uamuzi wako. Fanya uamuzi wako na uliamini kwa moyo wako wote. Yeye ana haki ya kuandika hili katika Maandiko. Ana haki ya yale anayosema. Ninaweza kuthibitisha hilo. Ninajua hajakosea. Mungu hulithibitisha.

271 Yeye hahitaji mtu yeyote kufasiri, aseme, "Hili ni *lile*, na Hili ni *lile*." Anasema atafanya, kisha analifanya, na hilo latosha. Yeye Ndiye anayejifasiria.

272 Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ni wangapi walio waaminio, basi? Inua mkono wako, useme, "Mimi ni mwaminio." Ninataka kila mwaminio hapa ndani asimame kwa miguu yake. Usiyeamini, endelea kuketi. Waaminio simameni kwa miguu yenu.

273 Katika mahakama hii, kabla haijaahirishwa, ninataka kumshukuru Bwana kwamba mahakama hii imefikia uamuzi. Baraza la wazee wa mahakama limefikia uamuzi huu, ya kwamba Yesu Kristo ana haki ya kuweka mambo haya katika

Neno Lake. Yanapofasiriwa vizuri sawasawa na Neno, ni ya Kweli. Ni wangapi wenu, enyi mahakama, wanaamini hilo? Inua mkono wako, useme, “Mbele za Mungu, ninaamini ya kwamba ni Kweli. Ninaamini ya kwamba ni Kweli.” Sasa, ni wangapi, mnapoiweka mikono yenu chini, wanasema, “Mimi ni mwaminio wa yale uliyosema. Ninaamini kwamba ni Ukweli mtupu. Ni Neno la Mungu”? Inua mkono wako. Vema.

274 Sasa nawatakeni, mnyoshe mikono kuivuka meza, na kumwekea mwaminio mwingine mkono. Nyosha mkono wako kuivuka meza, uweke juu ya mwaminio mwingine. Je! sisi ni waaminio? Yeye alisema nini? “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

275 Enyi mahakama, mmefanya maamuzi? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] “Uamuzi wangu umefikiwa.” Hiyo ni kweli, “Amina”? [“Amina.”] Kwamba Neno la Mungu ni kweli, “Amina”? [“Amina.”] Marko 16 ni ya kweli, “Amina”? [“Amina.”] Basi, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Itawabidi kupata afya. [“Amina.”] Yeye alisema hivyo, sivyo? [“Amina.”]

276 Sasa, jinsi unavyoomba kanisani, mwombee mtu uliyemwekea mikono. Wao wanakuombea. “Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Itakuwaje? Matendo yako, kuanzia saa hii na kuendelea, yatathibitisha jinsi uamuzi wako wa kweli ulivyo.

277 Sasa inamisha kichwa chako, kila mmoja wenu. Sasa mwombee mtu huyo uliyemwekea mikono yako.

278 Yesu Kristo wa Nazareti, naomba uzingatie jambo hili tena. Wanaume hawa na wanawake wamedai, kwa ushuhuda wao, ya kwamba wao ni waaminio. Wamesimama, nao wamewekeana mikono. Bwana, tunaliamini Neno Lako, ya kwamba katika siku hii kuu ya elimu, siku hii kuu ya—ya—ya kusonga mbele, ya maadili na—na mifumo yote ya elimu, hata hivyo, katikati ya hayo yote, Neno Lako linabaki kweli vile vile tu.

279 Nasi tumewaita mashahidi kwenye mahakama hii alasiri ya leo, Bwana, kukufanyia kesi ya haki; sio kesi ya dhihaka, si ya dhihaka kama uliyopewa na Herode, ama—ama—ama kama mmoja wa hao wengine. Tunakufanyia kesi ya haki hapa, na kuthibitisha. Na watu Wako wamefanya maamuzi yao, ya kwamba Neno la Mungu katika mwaka wa 1964, saa hii tunayoishi, ya kwamba Wewe ni Mungu tu kadiri ulivyowahi kuwa. Na kila Neno ulilioahidi ni Kweli. Nao wamewekeana mikono, kama waaminio. Wanaombeana.

280 Nawe ulisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Kamwe hukusema ni lini. Ulisema, “Watapata afya.” Sasa, hao wakiwa . . .

281 Huku nikiwa msimamizi, nao hawa watu wakiwa ni baraza la wazee wa mahakama, pia hakimu, wametoa ushahidi kwa jambo hili, Bwana, kwa kusogezana mikono, na kuombeana.

282 Sasa, matendo yao baada ya hapa hakika yatathibitisha kilicho uamuzi wao. Jalia kusiweko na lalamiko moja miongoni mwao, tena, la kuwa wagonjwa wa maradhi haya, ama chochote kinachowasumbua sasa. Jalia wajue ya kwamba Mungu aliahidi ya kwamba atalitenda.

283 Wakati mwingine Yeye hukawia, kama alivyofanya katika siku za Nuhu, alivyofanya katika siku za Musa, alivyofanya katika siku zote. Bali Yeye—Yeye kamwe hakuwaambia Wapentekoste, "Pandeni mwende kwenye mji wa Yerusalemu, katika saa ishirini na nne nitawapa Roho Mtakatifu." Alisema, "Ngojeni pale mpaka mtakapovikwa uwezo utokao Juu." Kamwe hakusema, "Siku moja, siku mbili, siku kumi." Alisema, "Kaeni mpaka mtakapovikwa uwezo." Bwana, walikaa mpaka ushahidi ukanena kupitia wao, kwamba ilikuwa ni Roho Mtakatifu wa Mungu.

284 Sasa, jalia watu hawa, ambao wamewekeana mikono, waliosimama, mahakama hii alasiri ya leo, Mbele za Mungu, Mbele za Neno Lake sawasawa na nilivyolisoma. Nasi tulishuhudia jambo hili, ya kwamba tunaamini ya kwamba Yeye hulitimiza Neno Lake. Basi jalia kila mmoja aponywe, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

285 Sasa, ninyi nyote mnaoamini hilo, tangu wakati huu, kwamba mwaminio aliyesimama kwa miguu yake kama mwaminio, nawe ni mwaminio, kwamba umeshuhudia na kutoa ushahidi mbele ya mahakama hii alasiri ya leo ya kwamba unaamini kwamba Yeye ni mwenye haki na hulitimiza Neno Lake. Haidhuru litakawia muda gani, halina budi kutimia. Unaamini hilo? Inua mkono wako. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnalikubali? ["Amina."] Mungu awabariki. Ninaliamini kwa moyo wangu wote.

Sasa hebu na tuviinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

286 Je! kuna mtu hapa ndani ambaye amekuwa asiyeamini, mtu ambaye si Mkristo? Ninataka kukupa nafasi ya kuja hapa kwenye hii, mbele ya mahakama hii, na kuungama, na kusema, "Nimekuwa mwenye kushuku, maishani mwangu mwote. Lakini, tangu siku hii na kuendelea, ninamkubali Yesu Kristo."

287 Ninajua ya kwamba Biblia ilisema, kwamba, "Katika siku, kama ilivyokuwa, katika siku za—za Yona, aliyekuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku."

Walimwambia, "Tupe ishara."

288 Akasema, "Kizazi kiovu na cha zinaa, kizazi cha Sodoma, kinatafuta ishara, nao wataipata. Watapata ishara. Kwa kuwa kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi, siku tatu mchana na usiku, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuwa katika moyo wa nchi." Wanafunzi hawa tunaosoma habari zao, walikuwa wakielewa vibaya, wakati wasingewaamini hao waliokuwa wamemwona baada ya kufufuka katika wafu.

289 Tumemwona. Tunajua kwamba ni kweli. Amefufuka katika wafu. Tunaamini hilo. Nasi tunaishi katika siku kama ilivyokuwa katika siku za—za Yona, wakati miji ilikuwa imepotoshwa na maovu. Ndipo Yona akajitokeza, kutoka katika tumbo la nyangumi, kama mtu anayetoka kwa wafu. Na, leo hii, tunaamini Yesu Kristo amefufuka katika wafu na anajitambulisha kote katika wakati wa kanisa kama Mwana wa Mungu, na sasa anaijaza, anatimiza ahadi Yake katika siku za mwisho, kujifunua Mwenyewe kwa Uzao wa kifalme wa Ibrahimu, kama Mwana wa Adamu.

290 Mungu awabariki. Huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa, kimya na kwa kicho, tunapoimba ubeti mmoja, *Nampenda*. "Nampenda kwani alinipenda kwanza." Na endapo wewe si Mkristo, nawe unataka kuwa mmoja, na kuchukua msimamo wako usiku wa leo pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa, katika siku hii ya uovu kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, njoo huku wakati tukiimba, huku vichwa vyetu vimeinamishwa na kila mtu akiomba.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

291 Sasa hebu na tuendelee kuviinamisha vichwa vyetu, sasa, tunapovumisha. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nampenda*—Mh.]

292 Liwazie. Liwazie. Unaweza kujitikisa kidogo tu? Mungu yeye yule aliyefanya ahadi hiyo, Yeye yupo hapa, akiitambulisha, moja kwa moja duniani leo hii, akiithibitisha. Haya hapa Maandiko Yake. Hakuna mtu anayepaswa kuyafasiri. Yamefasiriwa tayari. Naye aliununua wokovu wangu. Hivi hamtalikubali?

[Ndugu Branham anaendelea kuvumisha *Nampenda*—Mh.]

293 Sasa, kama wewe tayari ni Mkristo, nawe ungetaka kuishi karibu zaidi na Mungu, hebu na tuiinue mikono yenu tunapouimba tena, huku vichwa vyetu vimeinamishwa. Unataka kutembea karibu zaidi na Mungu; unaamini kwamba hii ni Kweli, kwamba tunaishi katika siku za mwisho. "Na . . . "

294 Mungu awe pamoja nawe, rafiki. Usikose. Usikose. Mwamini. Nampenda. Maanisha kwa moyo wako wote sasa. Jisalimishe. Yeye ni Neno, Neno la wakati huu.

. . . -linipenda kwanza . . . ? . . .

Kesi SWA64-0427
(A Trial)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatatu jioni, tarehe 27 Aprili, 1964, kwa ajili ya dhifa ya Ushirika wa Kimataifa wa Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Ramada Inn huko Tucson, Arizona, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org